epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
Jumanne Novemba 5, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581851
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

# Makalla: Ukikatwa CCM kaa kimya



• **Awaonya** wagombea wake "safari hii hakuna kupita bila kupingwa"...*Endelea ukurasa 2*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika ufunguzi wa Mkutano wa Tisa wa Mwaka wa Mtandao wa Wasimamizi wa Mameneja Rasilimali Watu katika Sekta ya Umma uliofanyika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) jana. **PICHA: OWM**

## Mfumo wa elimu nchini wakosolewa hautoi majibu ya matatizo

UKURASA 4

UKURASA WA 4

**Tundu** Lissu atoa sababu za kutojiandikisha kupiga kura

UKURASA WA 15

**Wabunge** waibana serikali ilipe madeni sugu ya wazabuni

UKURASA WA 2

**Aliyeshtakiwa** kumchoma mkewe kwa magunia ya mkaa ana shida ya akili - Ripoti





## Maziko ya Musuguri yawakutanisha majenerali

UKURASA 3

Nipashe WhatsApp Chaneli

Skani hapa kutembelea chaneli yetu

# Makalla: Ukikatwa CCM kaa kimya

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, amewataka wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi kuwa na subira.

Amesema watakaokatwa licha ya kushinda kura za maoni, wasiseme neno, badala yake wawe na uvumilivu kwa kuwa muda wao utafika, huku akiwatakia heri waliohamia vyama vingine, akidai kuwa ni suala la muda tu.

Mwenezi huyo pia amesema uchaguzi wa awamu hii hauna kupita bila kupingwa, hivyo wagombea wa wanachama wa chama hicho wasibweteke, akisisitiza wako imara na hawatalala.



Makalla aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa mkutano wa chama wilayani Kinondoni, akisisitiza watahakikisha hata pale watakapokuwa peke yao, watafanya kampeni na kuhakikisha wagombea wao wanapata kura za "ndio".

"Anayesubiri kumwangusha mgombea wa CCM kwa kura za "hapana" ni sawa na mtu anayesubiri ndege bandarini badala ya 'Airport' (uwanja wa ndege). Wana CCM nchini kote tuchangamke, hakuna neno 'mama' tukamilishe hiyo kazi, mahali patakapothibitika tupo sisi tutafanya kampeni ya kutosha, wagombea wetu wote wapite kwa kishindo.

"Niwaombe tuendelee kufuatilia viongozi wetu wa matawi, kata, wilaya na mkoa, michakato inayoendelea sasa ya kupeleka wagombea katika maeneo hayo, itakapofika Novemba 21, mwaka huu tuanze kampeni za kistaarabu za kunadi mafanikio tuliyonayo na utekelezaji ilani ya uchaguzi. Kazi zilizofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan ni mtaji tosha wa kuipa CCM ushindi," alisema Makalla.

Aliongeza kuwa walifanya hamasa kubwa ya uandikishaji iliyofanikisha zaidi ya watu milioni tatu kuandikishwa ndani ya mkoa wa Dar es Salaam pekee, akieleza kuwa hamasa hiyo itakayotumika kufanya kampeni muda utakapofika, ifanywe kuwasisitiza wananchi kutoishia kwenye kijiandikisha badala yake wajitokeze pia kupiga kura.

Makalla alieleza kuwa chama hicho kinaamini kwamba Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni muhimu, hivyo wamejiwekea utaratimu maalumu ambao utafanikisha kupata zaidi ya viongozi 500 watakaogombea katika maeneo mbalimbali kote nchini, akiwasisitiza kuonesha taswira nzuri kwa kuwa wameaminiwa.

Aliwapongeza baadhi ya wagombea ambao majina yao yalikatwa na wanaendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali za chama hicho, akijitolea mfano yeye mwenyewe kwamba kuna kipindi aligombea na kushinda kwa kishindo lakini jina lake halikurudi.

"Tunawatakia kila la heri waliokosa uvumilivu, wako ambao hata uteuzi haujafanyika wakahamia mtaa wa pili siku ya tatu wakageuza tena CCM, niwape salamu hao waliowaokoteza tumewaazima tu wagombea, watarudi Chama Cha Mapinduzi.

"Kuna wengine hata vikao hatujakaa niliona wanakaribishwa siku mbili jamaa akarudisha kadi akarudi CCM, hivyo niwaombe kuweni watulivu, tuna uchaguzi mwakani," alisema Makalla.

# Ripoti: Aliyeshtakiwa kumchoma mkewe kwa magunia ya mkaa ana shida ya akili

**Na Grace Gurisha**

RIPOTI kutoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili, Mirembe, imeeleza kuwa mfanyabiashara Khamis Luwonga (38), anayetuhumiwa kumuua mkewe, Naomi Marijani na kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa, wakati anafanya tukio hilo la mauaji alikuwa ana shida ya akili.

Aidha, mashahidi wawili wa upande wa mashtaka (askari polisi) wamedai kuwa wakati mshtakiwa huyo alipokwenda Kituo cha Polisi cha Mji Mwema na Kituo cha Polisi Kigamboni, alikuwa akionekana mtu mwenye akili timamu.

Taarifa hiyo, ilitolewa jana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Mwasiti Athuman, mbele ya Jaji Hamidu Mwanga wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kusikilizwa.

Wakili Athuman alidai kuwa katika kikao cha mwisho Mahakama ilielekeza mshtakiwa apelekwe kwenye Hospitali ya Afya ya Akili kuangalia wakati anafanya tukio hilo alikuwa ana akili timamu au la.

Alidai ripoti ya kitababu ya hospitali hiyo ya Septemba 26, 2024 katika ukurasa wake wa tatu inaeleza kuwa baada ya mshtakiwa kufanyiwa uchunguzi wa kitaalamu waliona ana ugonjwa wa kifafa na alipewa dawa.

Pia, alidai kuwa ilionekana mshtakiwa huyo wakati anafanya tukio hilo alikuwa ana shida ya akili, kwa kuwa ushahidi huo ni wa upande wa utetezi, wapo tayari kuendelea na usikilizwaji na wana mashahidi wawili.

Baada ya kudai hayo, Wakili wa mshtakiwa Mohamed Majaliwa akisaidiana na Zidadi Mikidadi, Jaqum Kamuli, Jacob Mwambasi na Fatuma Abdul, alidai kuwa hawana pingamizi na hilo kwa sababu ripoti hiyo inaingia kwenye mwenendo wa kesi, kwa hiyo wapo tayari kuendelea.

Shahidi wa kwanza, Salama Haji Jecha (53) ambaye ni mstaafu wa Jeshi la Polisi kutoka Kituo kidogo cha Polisi Mji Mwema, alidai mahakamani jinsi alivyompokea mshtakiwa kituoni hapo Mei 19, 2019.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Eric Kamala, Jecha alidai kuwa tarehe hiyo majira ya asubuhi alikuwa kituoni akiendelea na majukumu yake ya kazi, saa 3:29 asubuhi alimpokea mshtakiwa ambaye alijitambulisha anaitwa Hamis, akatoa taarifa ya kupotelewa na mke wake Naomi Marijani.

"Nilimuuliza ni muda gani mke wake hayupo nyumbani, akasema ni wiki moja, nikamfungulia taarifa zake nikampa RB nikamweleza kama hadi kesho yake hajarudi aende akaripoti kituo kikubwa cha Polisi Kigamboni," alidai Jecha.

Pia, alidai kuwa mshtakiwa huyo alipokwenda kituoni hapo alikuwa mzima wa afya na mwonekano wake alionekana hakuwa na tatizo lolote la kiafya.

Hata hivyo, Julai 16, 2019 alipokuwa kazini anakumbuka alikwenda Afande James akamweleza kwamba kuna mwananchi alikwenda kutoa taarifa kuwa mke wake amepotea, sio kweli, amemuua mwenyewe.

Akijibu maswali ya Wakili Majaliwa, Jecha alidai hakufungua jalada, alimpa mshtakiwa RB na taarifa zake aliziandika kwenye kitabu cha kumbukumbu cha polisi na pia hakumchukua maelezo.

"Mbali na mimi sijui nani mwingine ambaye alishughulikia suala lake, kazi yangu ni kupokea taarifa na kupiga simu kwa wakubwa waliokuwapo Kituo cha Polisi Kigamboni," alidai.

Pia, akijibu swali la Mikidadi kwamba ana utaalamu wowote wa kitabibu hadi kufikia hatua ya kudai kuwa mshtakiwa hakuwa na tatizo lolote, alidai hana utaalamu huo.

Shahidi wa pili E 7870 D/ Sajenti Audifas (53), mkazi wa Kagera, Dar es Salaam alidai Juni 11, 2019 akiwa katika Kituo cha Polisi Kigamboni alimpokea mshtakiwa akimweleza ana shida, ana namba ya simu ya mke wake, anataka amwangalizie yuko wapi kwa sababu hayuko nyumbani.

"Nikamwambia siwezi, anatakiwa afungue kesi kwanza ili apate namba ya kesi, ndiyo tukafungua ya kutelekeza mtoto wa miaka sita. Na mara nyingi alikuwa anaonakana kama mteja kwa sababu alikuwa anakwenda kituoni hapo kuhusu kesi za viwanja, wakati wote huo alionekana na afya njema," alidai.

Akijibu maswali ya upande wa utetezi, shahidi huyo alidai kuwa hakuleta maelezo ya mshtakiwa mahakamani kwa sababu hayajabishaniwa, lakini kama yatahitajika atayaleta.

Kwa maoni: +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz

# Chanzo kifo mmiliki wa Chako ni Chako chatajwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma, limetaja chanzo cha ajali iliyosababisha kifo cha mmiliki wa baa ya Chako ni Chako na Epic zilizoko jijini hapo, Honorath Mkoyi, kuwa ni mwendo kasi na kutozingatia usalama barabarani.

Mmiliki huyo alipata ajali hiyo juzi majira ya saa 9:00 usiku akiwa anaendesha gari aina Toyota Brevis lenye namba za usajili T 781 DMS, barabara ya wajenzi kuelekea Swaswa baada ya kubadili mwelekeo na kugonga mti kutokana na mwendokasi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo alisema, Honorati Makoyi, alifariki dunia nusu saa baada ya kufikishwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

Kamanda, alisema dereva wa gari hilo ambaye ni marehemu alikuwa akiendesha kwa kasi jambo lililosababisha gari hilo kubadili mwelekeo kutoka kushoto kuelekea kulia na kugonga mti baada ya kushindwa kulimudu na kusababisha ajali hiyo iliochukua uhai wake.

"Chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi uliosababishwa na dereva nawasihi madereva wawapo barabarani kuwa makini na sheria za uendeshaji ili kuepuka kusababisha ajali," alisema Kamanda Katabazi.

Aidha, alisema madereva wamekuwa na tabia ya kujisahau barabarani ikiwamo kuendesha mwendo kasi na kuwataka abiria kutoa taarifa kwa jeshi hilo wanapoona dereva anaendesha kwa mwendo kasi.

"Naomba madereva kufuata sheria za usalama barabarani ikiwamo kuwa makini na aina ya uendeshaji wa gari, hakuna haja ya kuendesha spidi kubwa bila sababu yoyote," alisema Kamanda Katabazi.

Aliwataka abiria wanaopanda vyombo vya moto kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi pale wanapoona dereva wa gari anakwenda kinyume na sheria za uendeshaji barabarani.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi mkoani hapa linamshikilia dereva wa gari aina ya Toyota Rav 4 lenye namba za usajili T 156 EJJ kutokana na kusababisha ajali iliyojeruhi watu 10 baada ya kugonga gari moja, bajaji na pikipiki mbili katika eneo la Makulu, jijini hapa.

Katabazi alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa gari aina ya Rav 4 kuendesha chombo cha moto akiwa amelewa.

Ofisa Uhusiano na Mawasiliano wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Lovenes Meena, alisema wamepokea majeruhi 10 wa ajali hiyo wakiwamo wanawake sita na wanaume wanne na wote hali zao zinaendelea vizuri.

"Majeruhi wa ajali hiyo wote wanaendelea vizuri na wanaendelea kupatiwa matibabu hospitalini hapa na hakuna kifo," alisema Meena.

# Maziko ya Musuguri yawakutanisha majenerali

**Na Waandishi Wetu**

MWILI wa Mkuu wa Majeshi mstaafu, Jenerali David Musuguri umezikwa kijijini kwao wilayani Butiama, mkoani Mara alikoishi kwa miaka 36 baada ya kutumikia jeshini kwa miaka 44.

Hatua ya kuweka mwili wake kaburini ilikuwa jana saa 6:41 mchana, kukishuhudiwa orodha ya waombolezaji inayowajumuisha Wakuu wa Majeshi wastaafu waliompokea kama vile Majenerali Robert Mboma, George Waitara na Venance Mabeyo.

Sambamba na hilo, ni tukio lililowakusanya makamanda wa ngazi za juu mbalimbali wastaafu wa muda mrefu na mfupi, huku tukio likichukua saa kadhaa, likitawaliwa na sanaa zote za kijeshi na kiimani, likiongozwa na Askofu wa Jimbo Katoliki Musoma, Michael Msonganzila.

Aidha, kiongozi wa kimila aliyewakilisha kundi la maisha yake mapya ya miongo mitatu na nusu kijijini, alikuwa Chifu wa Kabila la Wazanaki, Edward Wanzagi.

Akiongoza ibada ya maziko ya mwili wa Jenerali Musuguri, Askofu Msonganzila alisema, "Ukisimuliwa vita ambavyo amevipitia ndani na nje ya nchi, mazingira ya vita ni ya kifo, kuua au kuuawa, lakini yeye alitoka mzima huko kote.

"Kwa Kiswahili wangesema 'ana Mungu wake' kwa sababu wengi walifariki dunia, wakiwamo viongozi na askari wa kawaida."

Mtazamo huo ulitolewa tafsiri nyingine na Mkuu wa Majeshi wa sasa, Jenerali Jacob Mkunda, ambaye anakiri hakuwahi kufanya naye kazi, lakini waliomtangulia wamempa sifa nyingi ya upendo jeshini na uzalendo.

Akizungumza baada ya ibada na taratibu za mazishi, Jenerali Mkunda alisema Jenerali Musuguri atakumbukwa si ndani tu ya Tanzania, bali pia nje ya Tanzania kutokana na mambo aliyoyafanya, akilitumikia Jeshi la King's African Rifles (KAR) pamoja na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ).

Alisema Jenerali Musuguri katika kipindi cha miaka 104 ya maisha yake, alitumia miaka 44 na siku 24 sawa asilimia 43 ya uhai wake katika utumishi wa umma kupitia JWTZ.

"Alitumikia jeshi kwa uhodari, ushujaa, uaminifu, utiifu na uadilifu mkubwa. Jenerali Musuguri alitumikia vyema Jeshi la King's African Rifles (KAR), alishiriki vita ya pili ya dunia chini ya majeshi ya Uingereza na washirika wake ambavyo vilimjenga, kumkomaza na kumpa uzoefu mkubwa na kuwa 'battle harden soldier', uzoefu aliotumia kulijenga jeshi la nchi mara na baada ya uhuru.

"Baada ya maasi ya mwaka 1964, jeshi liliundwa upya na kupatikana JWTZ ambako Jenerali Musuguri alitumikia akiwa katika vyeo na madaraka mbalimbali akiwa miongoni mwa waanzilishi wa jeshi hili kisha kupandishwa vyeo na kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi mwaka 1980 na kustaafu utumishi mwaka 1988," alisema Jenerali Mkunda.

Alisema kuwa Jenerali Musuguri ni miongoni mwa watu walioshiriki kulijenga na kuliimarisha jeshi hilo, akihudumu katika vikosi vyote vya mwanzo ambavyo ni battalion 1, 2 na 3 na baadaye kuziongoza brigedi 201 na 202 na kisha kamanda wa divisheni ya 20 ambako aliteuliwa kuwa kamanda wa operesheni katika Vita vya Kagera baada ya kukombolewa kwa ardhi ya Tanzania. Hivyo, kusimamia mipango yote ya vita hiyo.

Maziko ya mwili wa Jenerali Musuguri yaliongozwa kiserikali na Naibu Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko.

Akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika maziko hayo, Naibu Waziri Mkuu Biteko alisema taifa litaendelea kumwenzi kwa ujasili wake Jenerali Musuguri ikiwa ni pamoja na kujitoa kujiunga jeshini akiwa na umri mdogo wa miaka 22 chini ya jeshi la wakoloni.

"Alihakikisha Tanzania inabaki kuwa na amani, usalama na mshikamano, hivyo kama familia na Watanzania wote niwaase tuendelee kushikilia imani yake pamoja na maono yake hasa katika kipindi hiki cha uchaguzi, tuishi bila kuharibu amani ya taifa letu," alisema Dk. Biteko.

Chifu wa Kabila la Wazanaki, Edward Wanzagi, alisema kabila hilo ndilo limemzaa na kumlea Musuguri ambaye alikuwa ni mtu muhimu mwenye kipaji, uwezo, utu, uadilifu na haiba ya kipekee.

Alisema Jenerali Musuguri aliwasaidia kuondokana na migogoro ya mipaka kutokana na kuyafahamu ipasavyo maeneo ya mipaka yao, hivyo kuomba mipaka hiyo iendelee kuheshimiwa.

Jenerali Musuguri alizaliwa mwaka 1920 wilayani Butiama na kujiunga na Jeshi la King's African Rifles (KAR) mwaka 1942 ambalo alilitumikia mpaka kipindi cha maasi na kuanzishwa JWTZ mwaka 1964 kisha kuongoza Vita vya Kagera na baadaye kuteuliwa kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi mwaka 1980, nafasi aliyoitumikia hadi anastaafu mwaka 1988.

Jenerali Musuguri alifariki Dunia Oktoba 29 mwaka huu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, mkoani Mwanza alikokuwa anapatiwa matibabu.

Wakuu wa majeshi nchini tangu kuundwa JWTZ ni Majenerali Mirisho Sarakikya (1964-1974), Twalipo (1974-1980), Musuguri (1980-1988), Mwita Kiaro (1988-1994), Waitara (2001-2007), Mwamunyange (2007-2017), Mabeyo (2017-2022) na wa sasa Mkunda.

***Imeandaliwa na Vitus Audax na Neema Emmanuel**




HABARI KITAIFA



Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, akizungumza na wanachama wa chama hicho, Wilaya ya Kinondoni, katika mkutano uliofanyika jana mkoani Dar es Salaam, ambako alitoa wito kwa wananchi kuwa kujiandikisha hakutoshi badala yake wajitokeze pia kupiga kura katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika hivi karibuni. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Tundu Lissu ataja sababu kutojiandikisha kupiga kura

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ameweka wazi sababu iliyochangia kushindwa kujiandikisha katika Daftari la Wakaazi ili kupiga kura katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Kauli hiyo ya Lissu imekuja ikiwa ni siku chache tangu Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi(CCM), Amos Makalla, atamke kwamba kiongozi huyo mkuu ndani ya CHADEMA hakujiandikisha na "ameweka rekodi yake ya kiongozi wa chama kutokupiga kura katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa".

"Sikujiandikisha kwenye daftari kwa sababu niliondoka Oktoba 2 kuja Ubelgiji kufuatilia mambo yangu ya kufungua kesi dhidi ya kampuni moja ya simu, nilitarajia kuwa ningerudi mapema lakini haikuwezekana, bado nipo huku," alisema Lissu.

Oktoba 22, mwaka huu, akipokea ripoti ya uandikishwaji mkoa wa Dar es Salaam, Makalla alisema alitarajia kiongozi huyo mkuu ndani ya chama chake, angeonesha mfano kwa wanachama na wafuasi wake kama ambavyo viongozi wengine wamefanya kwa kuwa mstari wa mbele kujiandikisha katika daftari hilo.

"Nionesheni mahali popote Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu alipojiandikisha. Atapataje uhalali wa kuhoji kuhusu kura, kuhusu haki ya kupiga kura, anapeleka 'message' (ujumbe) gani kwa wafuasi wake? Uongozi ni mfano.

"Inakuwaje kiongozi ambaye ni mwanasheria, anajua haki, anajua demokrasia, anaikataa haki yake ya kupiga kura? Kwa hiyo, inaingia katika rekodi kuwa hatopiga kura katika nchi hii kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, lakini tutarajie kelele za kuhoji matokeo, wakati hata kura yake hana," alisema hivyo Makalla Oktoba 22, mwaka huu.

Akijibu hoja hiyo, Lissu alisema: "Kutokujiandikisha kupiga kura hakumwondolei mtu yeyote haki ya kuzungumza chochote kuhusiana na utaratibu wa uchaguzi husika, kama ambavyo haimwondolei mtu yeyote haki ya kuzungumzia mambo yoyote yanayohusu umma katika nchi yetu.

"Uchaguzi wetu unazungumziwa si tu na watu wanaopiga kura kwenye uchaguzi huo, isipokuwa unazungumziwa pia na jumuiya ya kimataifa. Ndio maana huwa wanakuja watu kutoka nje ya nchi kuja kutazama uchaguzi huo kama ni huru na haki kiasi gani.

"Uchaguzi huo unazungumzwa na kwenye vyombo vya habari vya ndani na nje, na si kila mtu anayezungumzia uchaguzi wetu ni mtu mwenye haki ya kupiga kura au ya kuchaguliwa," alisema Lissu.

Mtaalamu huyo wa sheria alisema kuwa kabla ya kuondoka kwenda Ubelgiji Oktoba 2 mwaka huu, alikuwa akitoa elimu kwa viongozi wa chama chake kwenye Jimbo la Kibamba, hivyo katika uchaguzi ambao chama chake kinaweka nguvu, ni pamoja na huo wa serikali za mitaa.

"Ile siku niliyoondoka, kabla sijaenda uwanja wa ndege kusafiri, nilikuwa ninafanya mafunzo ya viongozi na watia nia wa kugombea uchaguzi huo katika Jimbo la Kibamba la mkoa wa Dar es Salaam.

"Hiyo inakuonesha ni jinsi gani ambavyo ninautilia maanani uchaguzi huo, na hayo mafunzo nimeyafanya si Kibamba tu, nimeyafanya kwa viongozi wa ngazi za kanda, makao makuu ya chama, nimeyafanya jimboni kwangu Singida Mashariki na nimeyafanya Singida Kaskazini.

"Kwa hiyo, mtu anayesema sitilii maanani kwa sababu tu nimeshindwa kujiandikisha kupiga kura kutokana na hayo niliyoeleza..." alisema Lissu.

# Mfumo wa elimu nchini wakosolewa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Kuteuliwa, Shamsi Vuai Nahodha, amekosoa mfumo wa elimu kuwa ni tatizo kutokana na masomo kufundishwa "kijumla jumla" na kutokuwa na uhusiano wa moja kwa moja na kupunguza umaskini.

Akichangia mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26, alisema njia mwafaka ya kuongeza tija katika uzalishaji iwe katika sekta ya kilimo au viwanda ni kuwekeza kwenye elimu bora inayosisitiza ufundi na ugunduzi.

"Ni bahati mbaya elimu yetu bado haikidhi kiwango hicho cha ubora na mara nyingi tunafundisha masomo ya jumla badala ya yanayosisitiza ujuzi, weledi na umahiri, tunatumia wastani wa Sh. bilioni 500 kila mwaka kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu na fedha hizi mchango wake ni mdogo katika kukuza uchumi," alisema.

"Tatizo letu ni nini, tunafundisha masomo ya jumla jumla ambayo hayana uhusiano wa moja kwa moja katika kupunguza umaskini, nilitarajia tungefundisha usimamizi wa mipango, usimamizi wa maendeleo, usimamizi wa rasilimali watu, usimamizi wa viwanda na usimamizi wa sekta ya afya na ndiyo ambayo yanahusiana na kupunguza umasikini."

Vile vile, alisema alitarajia wafundishwe masomo ya ukalimani, ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni ili wataf-sirie wataalamu nchi za ughaibuni na kwa upande wa teknolojia alitarajia wafundishwe vijana masuala ya sayansi ya data na akili bandia.

Alisema Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) kina shule nzima ya teknolojia ya habari na wakati huo huo Wizara ya Habari na Teknolojia ya Habari inajenga chuo cha umahiri cha teknolojia na Tehama na kudai kuwa ni matumizi mabaya ya fedha.

"Kwa maoni yangu, haya ni matumizi mabaya sana ya rasilimali za taifa, ingekuwa vizuri kama taifa tungegawa vyuo vikuu kulingana na weledi na ubobezi wa masomo, UDOM kingefundisha masuala ya sayansi, teknolojia na uvumbuzi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kingefundisha masomo ya Sayansi ya Jamii, Muhimbili kikaendelea kama kilivyo na SUA kikaendelea kama kilivyo," alisema.

Alisema pamoja na Wizara ya Elimu kuwa na dhamira ya kufundisha masomo ya ufundi na amali katika shule zote za sekondari na kuwa na vyuo vya VETA Tanzania nzima, lakini uwezo haupo wa kutekeleza jambo hilo.

**MATUMIZI MZIGO**

Alisema baadhi ya matumizi ya serikali kwa maoni yake yanaibebesha serikali mzigo mkubwa badala ya kusaidia kuongeza tija.

"Mfano Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Maliasili, Wizara ya Maji wananunua mitambo inayofanana na wote wanafanya kazi ya kuchimba mabwawa na kutengeneza barabara."

"Baada ya muda mfupi tu, vifaa vinaanza kutelekezwa porini kwa sababu ya gharama za mafuta na gharama za matengenezo zimekuwa kubwa sana badala ya vifaa hivyo kuwekwa sehemu moja na kila anayehitaji atakodi," alisema.

Alisema licha ya Wizara ya Kilimo kupatiwa wastani wa Sh. trilioni moja kila mwaka kwa ajili ya maendeleo ya kilimo, tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo bado iko chini sana.

Naye Mbunge wa Mahonda (CCM), Abdullah Ali Mwinyi, alisema elimu ya chuo kikuu haina umuhimu mkubwa kwenye ajira na kampuni zote kubwa kwa kuwa wanaangalia suala la ujuzi.

**MIRADI KIMKAKATI**

Mbunge wa Kuteuliwa, Prof. Shukrani Manya alitaka utashi uliotumika kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa ya Reli ya Kisasa (SGR) na Bwawa la Mwalimu Nyerere ufanyike kwenye miradi ya Liganga na Mradi wa Kusindika na Kuchakata Gesi (LNG).

Alisema mradi wa LNG ukikamilika au kuanza mapema ni kichocheo cha viwanda vya mbolea na kemikali na kuokoa fedha zinazotumika kuagiza mbolea nje ya nchi.

"Mradi wa Chuma wa Liganga umekuwa ukitajwa mwaka hadi mwaka kwenye mipango na bajeti ya serikali, tunajenga reli kwa kutumia chuma nyingi sana, kwa utashi ambao serikali imefanikisha kwa miradi mikubwa basi miradi hii mingine nayo ambayo imeendelea kuongelewa mwaka hadi mwaka, Prof. Mkumbo (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, huu mpango useme ni lini, tusiendelee kuwa tunahamisha, tunapanga, tuseme lini," alisema.

Kuhusu kubana matumizi fedha za uendeshaji, Prof. Manya alisema kutokana na kuwa na umeme unaotosheleza mahitaji, anapendekeza Mamlaka za Maji zipewe tariff maalum ya umeme ili kupunguza wananchi wapate maji kwa gharama nafuu.

Naye Mbunge wa Ludewa (CCM), Joseph Kamonga, aliomba serikali iongeze kasi ya utekelezaji kwenye mradi wa Liganga na mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma.

Mbunge wa Ndanda (CCM), Cecil Mwambe, alisema mradi wa Liganga na Mchuchuma kwa sasa ni zaidi ya miaka 50 tangu akiwa mdogo unaongelewa na kwamba kwa sasa wanataka waone utekelezaji wa mradi huo ili uwe na tija.

# PPRA yatoa mikataba 62,000 kwa wazabuni mfumo wa kielektroniki

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imesema mikataba 62,000 yenye thamani ya Sh. trilioni 10 imetolewa kwa wazabuni kupitia mfumo wa kielektroniki wa serikali wa Nest.

Mkurugenzi Mkuu, Denis Simba, alisema hayo katika kikao kazi na waandishi wa habari na wahariri kilichofanyika jijini Dar es Salaam, jana.

Simba alitoa takwimu hizo wakati akizungumzia mafanikio ya PPRA katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi mwaka huu cha uongozi wa serikali ya awamu ya sita.

"Mafanikio mbalimbali yamepatikana kupitia mabadiliko ya sheria kati ya mwaka 2001 hadi 2023," alisema Simba katika kikao hicho ambacho ni kwa mujibu wa maelezo ya Ofisi ya Msajli wa Hazina kwa taasisi zilizoko chini yake kuueleza umma, mafanikio, changamoto na matarajio ya kazi zinazotarajia kufanya kwa ajili ya kuwaletea maendeleo.

Alitaja mafanikio mengine kuwa ni kuendelea kuongezeka kwa kiwango cha ukidhi wa sheria, ununuzi wa umma kufanyika kwa njia ya kielektroniki;

Kuandaliwa na kuanza kutumika kwa kanuni za maadili kwa watumishi wa umma na wazabuni wanaoshiriki katika shughuli za ununuzi wa umma; Ununuzi wa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji, wasambazaji, mawakala wakubwa na kuongezeka kwa hadhi ya vitengo vya usimamizi wa ununuzi.

Akizungumzia changamoto, alizitaja kuwa ni bei kubwa za bidhaa, huduma na kandarasi ikilinganishwa na bei ya soko.

Kukosekana kwa viwango vya ukomo wa uidhinishaji wa zabuni, kukosekana kwa masuala ya ugavi katika sheria ya ununuzi.

Vilevile, alisema usimamizi hafifu wa mikataba ya ununuzi kutokana na ukosefu wa masharti mahsusi katika sheria kuhusu usimamizi wa mikataba;

Alisema changamoto zilizosababishwa kutungwa sheria mpya ni kutotofautisha masharti ya ununuzi kati ya taasisi za umma zinazojiendesha na zisizojiendesha kibiashara.

Alisema nyingine ni kutokuwapo kwa sharti la bei kikomo katika ununuzi wa umma, sheria kutokuwa na masharti ya ukomo wa thamani ya miradi, uandaaji wa taarifa ya ukaguzi wa kazi zilizofanyika, udhibiti wa ubora wa kazi iliyotekelezwa, viwango vya weledi na uzoefu wa watekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa utaratibu wa Force Account (akaunti ya papo kwa papo).

Alisema lengo la kufanya maboresho ya sheria yalikuwa ni kuondoa mwanya kwa taasisi kufanya ununuzi nje ya mfumo wa kielektroniki na kuwapo kwa taratibu za ununuzi kwa mashirika na taasisi za umma zinazojiendesha kibiashara.

Aidha, alisema kuwa maboresho ya sheria pia yalilenga ujumuisha masuala ya usimamizi wa ugavi, kuweka sehemu mahsusi kuhusu masuala ya usimamizi na utekelezaji wa mikataba ya ununuzi, bei kikomo, maboresho ya utaratibu wa akaunti ya papo kwa papo ikiwamo kuweka ukomo wa thamani.

Akizungumzia kuhusu malengo ya PPRA, alisema yatakuwa ni kuhakikisha taasisi za ununuzi zinatoa upendeleo kwa wazabuni wa ndani katika zabuni za bidhaa, kazi za ujenzi na huduma.

Awali aliyataja majukumu ya mamlaka hiyo kuwa ni kuishauri serikali, mamlaka za serikali za mitaa na vyombo vilivyoanzishwa kisheria kuhusu misingi na mienendo ya ununuzi na ugavi; kutoa taarifa juu ya utendaji kazi wa mifumo ya usimamizi wa ununuzi na ugavi katika Jamhuri ya Muungano na kushauri mabadiliko yanayohitajika.

Kudhibiti ununuzi wa washauri elekezi, washauri wa miradi na mtu binafsi kuhusiana na miradi ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Kuratibu na kutunza mfumo wa uchapishaji wa taarifa kuhusu fursa za ununuzi wa umma, tuzo na taarifa nyingine zozote zenye maslahi kwa umma kama itakavyoamuliwa na mamlaka.

Akizungumzia kuhusu fursa zilizopo katika sheria ya ununuzi wa umma namba 10 ya mwaka 2023 iliyoanza kutumika Julai mwaka huu, Simba, alisema imeweka fursa mbalimbali ikiwamo upendeleo wa kitaifa na kipekee kwa watu au kampuni za ndani.

Ushiriki wa kampuni na wataalamu wa ndani katika mikataba ya ushauri elekezi, matumizi ya wataalamu wa ndani katika mikataba ya kazi za ujenzi na huduma zisizo za ushauri elekezi.

Alisema PPRA imeziagiza taasisi nunuzi pamoja na mambo mengine kutenga asilimia 30 kwa ajili ya kunufaisha makundi maalumu ya wazawa, wakiwamo wanawake, vijana na wazee ili kuinua uchumi na kuondokana na umaskini.





## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi ambao orodha yao ipo hapa chini waliolipia viwanja kwa nyakati tofauti eneo la Kikombo Kitalu "DA" na "N" kupitia benki, ila taarifa zao zinamapungufu ya majina, namba ya kiwanja na kitalu wafike ya Halmashauri iliyopo Manispaa ya zamani sehemu ya **mauzo ya viwanja** kwa ajili ya kuhakiki taarifa zao.

Muda wa utekelezaji ni kuanzia tarehe 28 Oktoba, 2024 hadi tarehe 10 Novemba, 2024.

Kushindwa kufanya hivyo, umiliki huo hautatambulika tena.

**ORODHA YA MAJINA YENYE TAARIFA PUNGUFU**

| NA | JINA | MALIPO |
|---|---|---|
| 1. | Christopher Kasung | 10,000.00 |
| 2. | Mbaga lyombe | 1,000,000.00 |
| 3. | Veisi Maineko | 42,000.00 |
| 4. | George Abel Ngab | 300,000.00 |
| 5. | Ngalawe Hassan Ramadha | 6,931,641.00 |
| 6. | Esther Mpangala | 5,000,000.00 |
| 7. | Victoria Mgala | 400,000.00 |
| 8. | Godfrey K. Msongwe | 9,096,340.00 |
| 9. | Eliaza Mangera Wangwe | 5,148,000.00 |
| 10. | Florence N. Kebwe | 2,515,000.00 |
| 11. | Ali Hussein Habib | 338,300.00 |
| 12. | Joseph Lukumbika | 265,000.00 |
| 13. | Rosina J Delima | 2,249,554.00 |
| 14. | Kelvin Mlambalamba | 1,200,000.00 |
| 15. | Starphod Marwa | 1,000,000.00 |
| 16. | Ally H. Thabit | 3,000,000.00 |
| 17. | Mariam Tawakel | 10,000.00 |
| 18. | Jeremia Baha | 255,000.00 |
| 19. | Shani Mwaruka | 400,000.00 |
| 20. | Ramadhan N Simba | 50,000.00 |
| 21. | Ally Habiba Thabit | 3,000,000.00 |
| 22. | Job Ndalo | 100,000.00 |
| 23. | Giligoli A Ndaro | 100,000.00 |
| 24. | Gloria Reuben Ndaro | 80,000.00 |
| 25. | Magreth W Luma | 10,000.00 |
| 26. | Chedi Ng'enda | 21,729,382.00 |
| 27. | Sospeter N Marco | 2,500,000.00 |
| 28. | Geophrey Mtweve | 1,150,000.00 |
| 29. | Leonary Kimario | 24,000.00 |
| 30. | Lilian Sebastian | 1,625,000.00 |
| 31. | Anna Elisamehe | 400,000.00 |
| 32. | Olais Peter | 300,000.00 |
| 33. | Mussa Deogratius Limb | 4,566,560.00 |
| 34. | Marium | 225,000.00 |
| 35. | Rainer | 4,607,934.00 |
| 36. | George | 100,000.00 |
| 37. | Jafari | 500,000.00 |
| 38. | Dann | 10,000.00 |
| 39. | Victoria | 1,015,000.00 |
| 40. | Jona | 50,000.00 |
| 41. | Alvin | 677,100.00 |
| 423. | Christina | 700,000.00 |
| 43. | Tina | 100,000.00 |
| 44. | Doreen | 300,000.00 |
| 45. | Kelvin | 1,500,000.00 |
| 46. | Innocent | 1,000,000.00 |
| 47. | Mabrouk | 100,000.00 |
| 48. | SHM | 1,000,000.00 |
| 49. | Khadija | 500,000.00 |
| 50. | Jackline | 40,000.00 |
| 51. | Zubeda | 100,000.00 |
| 52. | Kelvin | 250,000.00 |
| 53. | Antony | 180,000.00 |
| 54. | Stanley | 3,500,000.00 |
| 55. | Kelvin | 250,000.00 |
| 56. | | 2,000,000.00 |
| 57 | | 220,000.00 |
| 58. | | 4,447,406.00 |
| 59. | | 2,000,000.00 |
| 60. | | 5,000,000.00 |
| 61. | | 1,566,355.00 |

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Nishati safi imepunguza biashara usafirishaji mkaa

**MIAKA** ya nyuma kabla ya kampeni ya matumizi ya nishati safi haijapamba moto, usafirishaji mkaa kutoka mikoani ulishamiri na uharibifu wa mazingira ulikuwa katika hali mbaya.

Kwa mifano michache kwa wanaopita Barabara ya Bagamoyo, ilikuwa huwezi kutembea bila kukutana na pikipiki au malori yaliyosheheni magunia ya mkaa.

Ukiangalia idadi ya magunia yaliyopakiwa kwenye malori hayo, utagundua ni jinsi gani misitu ilivyokuwa ikiangamia kwa kukatwa miti inayochomwa na kuwa mkaa.

Mbali na uharibifu wa mazingira, lakini matumizi ya kuni na mkaa yana athari kubwa katika afya za binadamu kutokana na moshi wanaouvuta.

Matumizi ya nishati safi ya gesi imesaidia kwa kiasi kikubwa kuepuka uchafuzi wa hewa ambao unasababisha uharibifu wa mazingira na pia kusababisha magonjwa mbalimbali.

Ulinzi wa afya ya mama, familia, mazingira na taifa dhidi ya mabadiliko ya tabianchi ni lazima uanzie jikoni.

Mkutano Mkuu wa Maboresho ya Serikali za Mitaa (TOA), ulieleza kuhusu tamanio la serikali kufikia asilimia 80 ya Watanzania wote kutumia nishati safi ifikapo mwaka 2034.

Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa kinara wa kutangaza matumizi ya nishati safi ya kupikia na lazima taifa lianze sasa kubadilisha nishati inayotumiwa kupikia.

Mara kwa mara anapokuwa kwenye majukwaa mbalimbali ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, Rais anasema huwezi kumaliza au kupunguza ukataji miti unaoangamiza misitu kama hutaligusa jiko.

Kampeni ya Rais imefanya mengi, Watanzania wameelezwa umuhimu wa matumizi ya teknolojia za kupikia zinazopunguza madhara kiafya, athari kwa mazingira na kijamii.

Na sasa Rais amelifikisha taifa kwenye kutekeleza Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia 2024 - 2034.

Analenga kaya zenye 'jiko safi na salama', ambayo asilimia 80 ya Watanzania watakuwa wanatumia jiko lenye nishati safi ya kupikia ifikapo 2034.

Pamoja na kuwaondoa kinamama katika matumizi ya kuni na mkaa na kutumia nishati safi, pia taasisi kubwa ambazo zinahudumia watu wengi kupata chakula, zinahimizwa kuhama kwenye matumizi ya kuni na mkaa na kuhamia kwenye nishati safi ili kupunguza uharibifu wa hewa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, ili kufanikiwa katika matumizi ya nishati safi ipo haja ya kuwa uhamasishaji wa kutumia majiko yanayotumia nishati safi na yapatikane kwa urahisi ili wanayoyahitaji wasipate vikwazo kwa kuyapata.

Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) inaeleza kuwa Tanzania Bara ina takribani kaya milioni 13.9.

Kufikia azma hiyo kaya zenye jiko safi na wakuu wa mikoa na wilaya wasimamie matumizi ya nishati safi ya kupikia na pia wizara na taasisi za umma kadhalika na sekta binafsi kuzingatia matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kulinda mazingira na kuepusha athari nyingi zinazotokana na kutumia nishati zisizo safi.

Mwaka jana Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira iliagiza taasisi zote zinazohudumia watu zaidi ya 100, ifikapo Januari, mwaka huu, ziache kutumia kuni na mkaa kupikia.


Ofisi ya Makamu wa Rais, katika mikakati yake inaeleza kuwa hilo limefanyika na taasisi nyingi zikiwamo za umma kuanzia Magereza, kambi za jeshi, shule za sekondari, vyuo vya ualimu na vikuu vimeanza kutumia nishati safi ya kupikia.

Pia, juhudi zinafanywa na kila taasisi inayohusika na nishati na katika mbio za Mwenge wa Uhuru, mwaka huu, ujumbe mkubwa unaobebwa ni uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi kupikia.

Uhamasishaji huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na kuepusha athari zinazosababishwa na hewa chafu inayotokana na kuvuta moshi mchafu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Mafanikio sayansi yanaanzia maabara

**KARIBU** kila sehemu wananchi wanaendelea kuhamasishwa kuchangia ujenzi wa miradi hasa majengo kwa ajili ya maabara za sekondari za kata.

Hayo yanafanyika, kwa sababu kila sekondari ya kata inapaswa kuwa na maabara tatu kwa masomo ya fizikia, kemia na bailojia ambazo ujenzi wake unajengwa kwa kushirikisha nguvu ya serikali na wananchi.

Pamoja na hayo, bado kuna changamoto mbalimbali ambazo kama hazitafanyiwa kazi haraka, huenda zikakwamisha juhudi zinazolenga kuhakikisha kila sekondari ya kata inakuwa na maabara tatu.

Miongoni mwa changamoto hizo ni baadhi ya shule kuwa na majengo na maabara zenyewe, lakini hazina wataalamu wa maabara hizo (Laboratory Technician), kwa ajili ya kuziendesha.

Uhaba huo wa wataalamu wa maabara, unaweza kurudisha nyuma jitihada za mafunzo kwa vitendo katika shule za sekondari licha ya kwamba kuna maabara katika shule hizo.

Ninaamini walimu wa masomo ya sayansi hawawezi kuwa na uwezo wa kutumia maabara kikamilifu, badala yake wataalamu wake ndio ambao wanahitajika ili wafundishe wanafunzi kwa ufasaha.

Wapo baadhi ya wanafunzi waliowahi kukaririwa na vyombo vya habari wakisema ukosefu wa wataalamu wa maabara katika shule zao unasababisha walimu wa masomo ya sayansi wageuke kuwa wataalamu wa maabara hizo, na kwamba hawana ujuzi wa kutosha wa kuzitumia.

Kwa kuwa katika kuboresha elimu jitihada mbalimbali zimekuwa zikifanywa na serikali, ikiwamo ujenzi wa madarasa, majengo ya maabara, ununuaji wa madawati na mahitaji mengine ya muhimu shuleni, ninadhani hata hili la wataalamu wa maabara lingepewa uzito zaidi.

Ninadhani ipo haja walimu wa masomo ya sayansi kupewa mafunzo ya jinsi ya kutumia maabara hizo ili waweze kufundisha wanafunzi, wakati serikali ikijiandaa kuweka wataalamu hao kila sekondari.

Wapo walimu ambao wanatajwa kutumia maabara hizo kufundisha wanafunzi. Ninadhani ndio wangepewa kipaumbele cha kufundishwa jinsi ya kutumia maabara hizo ili wasaidie wanafunzi.

Kama mwalimu anajaribu kufundisha kwa kutumia maabara hizo, maana yake ni kwamba ana uelewa nazo, hivyo akiongezewa ujuzi inaweza kuwa rahisi kwake kutumia kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi.

Hatua hiyo inaweza kusaidia kupunguza tatizo lililopo la ukosefu wa wataalamu hao ambalo linasababisha wanafunzi wasijifunze masomo ya sayansi kwa vitendo kama inavyotakiwa.

Iwapo walimu wataongezewa mafunzo ya utaalamu wa maabara wakijikita zaidi kwenye vitendo, watakuwa wamesaidia kupunguza tatizo la ukosefu wa wataalamu hao katika sekondari mbalimbali.

Ikumbukwe kuwa mwalimu anapohitimu mafunzo ya ualimu kama ni wa masomo ya sayansi, mara nyingi anakuwa anajua kufundisha kwa nadharia, hivyo hawezi kuwasaidia zaidi mwanafunzi kwa vitendo.

Lakini kwa kuwa ana uelewa wa kutumia maabara hizo, ninaamini akifundisha jinsi ya kuzitumia anaweza kuelewa kirahisi na hivyo kuwafundisha wanafunzi wake kwa vitendo

Kuendelea kuwapo kwa sekondari ambazo hazina wataalamu hao, kunaweza kukwamisha serikali katika mipango yake ya kuandaa wataalam wa fani mbalimbali wa baadaye.

Vilevile, kuwapo kwa wataalam hao shuleni kunasaidia wanafunzi kujifunza masomo ya sayansi kirahisi kwani watakuwa wanafanya kwa vitendo kuliko ilivyo sasa wanapojifunza kwa nadharia.

Ni muhimu kutambua kuwa kutumia walimu wasio na ujuzi katika maabara msaada wao kwa wanafunzi si mkubwa, hatua za haraka zinahitajika kufanikisha azma ya kuwa na mafanikio katika elimu kwa vitendo.

## Wabunge wataka viwanda vya vileo vitumie malighafi za ndani

**Na Moshi Lusonzo**

WAJUMBE wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Mifugo na Kilimo wamevitaka viwanda vinavyozalisha vileo nchini, kununua malighafi zinazotokana na mazao ya wakulima wa ndani badala ya kuagiza kutoka nje ya nchi.

Mwishoni mwa wiki wakati wa ziara yao katika kiwanda kinachozalisha bia cha Serengeti, wabunge hao walisema wakulima wengi wanaozalisha mazao ya mtama, mahindi na shayiri wanakosa soko kutokana na viwanda vya ndani kukataa kununua kwa madai ya kutokidhi ubora.

Mwenyekiti wa kamati hiyo ambaye ni Mbunge wa Njombe, Deo Mwanyika alisema kuna haja viwanda hivyo kununua mazao kwa wakulima wadogo katika mikoa inayozalisha mazao hayo kama njia ya kuongeza idadi na kuinua uchumi.

Alisema kiwango cha mazao wanayonunuliwa kwa wakuliwa wa ndani ni kidogo kulinganisha na kile wanachoagiza kutoka nje.

"Sisi kama wabunge na wawakilishi wa wananchi, tunahimiza viwanda vyetu kununua malighafi kutoka ndani ya nchi ili kuwafanya wakulima wetu wadogo wapate soko la uhakika na kuinua uchumi wao," alisema Mwanyika.

Awali, Mkurungezi wa SBL, Obinna Anyalebechi, aliwasilisha ombi kwa kamati hiyo kuhusu punguzo la kodi hadi kufikia Sh. 680 kwa lita moja ili kuwezesha kampuni hiyo kutumia asilimia 75 ya malighafi za nchini.

Anyalebechi alitaja punguzo la kodi ya ushuru la Sh. 620 kwa lita kwenye bia inayotengenezwa kutoka shayiri ya ndani kama mojawapo ya kodi zinazobagua.

Alisema punguzo wanalopendekeza litasaidia kuongeza kiwango cha uzalishaji mtama, mahindi na shayiri kwa wakuliwa wadogo wa ndani pamoja na kuipatia serikali pato kubwa linalotokana na kodi.

Mwanyika alisema kamati yake imesikia ombi hilo na itakwenda kujadili na kuandaa majadiliano ya wazi kwa viwanda vikubwa ili kuhakikisha vinaendelea kuwapo, pia kuongeza uzalishaji mazao kwa wakulima wa ndani.

Mjumbe wa kamati hiyo, Prof. Sospeter Muhongo, Mbunge wa Musoma Vijijini, ndiye aliyependekeza kuandaliwa mkutano wa wazalishaji wakubwa wa vileo, akisema njia hiyo ni bora zaidi ili kupata ulingano katika biashara na kuondoa hisia za kuhujumiana.

"Tukiwaita wote kwenye kamati na kila mmoja akatoa hoja zake, tutakuwa na majibu sahihi ya kuishauri serikali kuhusu punguzo la kodi na jinsi itakavyowanufaka wakulima wetu," alisema Prof. Muhongo.

Kamati hiyo iliendelea na ziara yake mwishoni mwa wiki katika viwanda mbalimbali mkoani Dar es Salaam kuangalia uendeshaji na changamoto wanazokabiliana nazo.

# Kamati yabaini tatizo utekelezaji miradi Mamlaka Serikali za Mitaa

**Na Jenifer Gilla**

KAMATI ya Bunge ya Bajeti imebaini itachukua miaka tisa na miezi mitatu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kukamilisha miradi viporo, hususani ujenzi wa vituo vya afya kutokana na ufinyu wa bajeti inayotokana na mapato ya ndani.

Vilevile, kamati hiyo imebaini nchi haipati fedha kutoka mifuko ya kimataifa ya kupambana na uharibifu wa mazingira kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo fedha za mfuko huo kujumuishwa kwenye bajeti ya mfuko mkuu na hivyo kutokuwa na uhakika kama zitaelekezwa kwenye shughuli ya mazingira.

Akisoma taarifa ya kamati hiyo mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa Kamati, Oran Njeza, alisema mwongozo unaelekeza serikali za mitaa kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha miradi viporo hususan vituo vilivyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.

Alisema hadi kufikia Machi mwaka huu, mahitaji ya ujenzi na ukamilishaji maboma hayo, yakiwamo ya zahanati, vituo vya afya, maabara na madarasa yaliyokuwapo, ni Sh. bilioni 267.66, kiasi ambacho ni kikubwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga kwa mapato ya ndani.

Mwenyekiti huyo alisema kufuatia hali hiyo, kamati imebaini itachukua takribani miaka tisa na miezi mitatu kwa mamlaka hizo kukamilisha maboma hayo kulingana na bajeti wanazotenga kila mwaka.

Alisema jambo hilo lilijadiliwa katika kikao cha Kamati ya Uongozi mwaka wa fedha wa 2023/24 na serikali iliahidi kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo.

Alisema ili kufanikisha ujenzi wa maboma hayo kwa wakati, kamati inaitaka serikali kutenga fedha kupitia ruzuku ya maendeleo inayotegemewa kurejeshwa kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Kiongozi huyo wa kamati alitaja sababu za nchi kutopata fedha kutoka mifuko ya kimataifa ya kupambana na uharibifu wa mazingira kwenda kwenye Mfuko wa Taifa wa Mazingira kuwa ni bodi ya mfuko huo kuwa bodi ya ushauri badala ya bodi ya uendeshaji.

Alitaja sababu nyingine kuwa ni mfuko huo kuwa chini ya idara iliyopo katika Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na si chini ya mamlaka au wakala.

Alisema pia fedha za mfuko kujumuishwa kwenye bajeti ya mfuko mkuu na hivyo kutokuwa na uhakika kwamba zitaelekezwa kwenye shughuli ya mazingira, mfuko kutokuwa na chanzo cha fedha cha uhakika na mfuko kutokuwa na watumishi wa kutosha kutokana na muundo wake.

"Kamati inaitaka serikali kufanya mapitio ya muundo wa usimamizi wa mfuko pamoja na kutafuta chanzo kwa ajili ya mfuko wa mazingira kwa sababu athari za mazingira si kihatarishi tena, bali zimekuwa janga," alisema.

Vilevile, alishauri serikali ione haja ya kutenga walau asilimia moja ya mapato yanayotokana na biashara ya hewa ukaa, ili yaelekezwe kwenye mfuko wa mazingira.

Kamati pia imebaini matumizi ya teknolojia ya akili mnemba nchini kuwa hafifu, hivyo kuzorotesha ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za serikali na kuachwa nyuma na kasi ya mabadiliko ya kidunia.

Alisema utafiti wao umebaini kuwa mpaka sasa ofisi ya mahakama ndio imepiga hatua katika matumizi hayo na kushauri serikali kuweka mkakati wa kuendeleza matumizi ya teknolojia hiyo katika sekta ya umma ili kuchochea ufanisi wa utekelezaji shughuli za serikali.

Vilevile, kamati ilishauri serikali kuelekeza kwa Ofisa Masuuli wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kwa kuwa ndio mamlaka inayohusika na mifumo ya serikali.

"Hali hiyo itarahisisha mifumo itakayoundwa kusomana na kutotawanya rasilimali fedha katika mafungu mbalimbali ambazo zinakwenda kutekeleza shughuli ambayo ingeweza kutekelezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao ambayo ndio yenye jukumu hilo," alisema.

Jana wabunge walianza kutoa maoni yao kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26.


RCC

**REYNOLDS CONSTRUCTION COMPANY (NIG.)LTD. (TANZANIA BRANCH)**

**Seize the Opportunity: Used Construction Equipment for Sale by Reynolds Construction Co. (Nig) Ltd – Tanzania Branch.**

**Issued this 04th November, 2024**

Reynolds Construction Co. (Nig) Ltd, a leader in civil engineering and infrastructure development, is offering a unique opportunity to purchase high-quality used construction machinery and equipment. This event presents a rare chance for interested buyers to acquire quality machinery. Here is what you need to know:

**Sale Terms and Conditions**

1. Bidder Registration and Security Deposit: Interested buyers must register and submit a refundable bid security deposit of Tsh. 1,000,000/= for each asset. Deposits are payable at Reynolds Construction Co. (Nig) Ltd Head Office Dar es salaam only. (The Bidder agrees to the seller that upon being awarded the assert, the security deposit shall be included in in his payments but if the bidder will cancel at his own will after being awarded the security deposit shall not be refunded.)

2. Duty Charges: Buyers are responsible for applicable duty charges. Estimated charges are indicative; buyers should verify these with the Tanzania Revenue Authority (TRA) before. purchasing.

3. Viewing Arrangements: Prospective buyers can arrange to view the equipment at their respective locations (Sululu ifakara Camp site). From 18th November, 2024 To 25th November, 2024.

   Site visits are available during business hours on weekdays and until midday on Saturdays. Visits must be scheduled in advance via email at **emmalucas25@yahoo.com** or by calling **+255 717293638.**

4. Tax Assessment and Duty Payment Approval: The disposing client must engage with TRA for tax assessment and duty payment approval before asset release.
5. Ownership Transfer Costs: Buyers are responsible for all costs associated with the transfer of ownership of the assets.

6. AS-it is, **WHERE IS** Basis: All assets are sold in their current condition and location without any warranties.

7. Additional Terms and Conditions: Further details will be provided in correspondence with interested buyers.

8. Bid Submission Deadline: Bids will be accepted at our Head Office at Plot 19, Manara Road – Ada Estate, Kinondoni P.O. Box 34653 Dar es Salaam from 26th November, 2024 To 28th November, 2024.

9. Cancelation of auction: The Bidders agrees to the seller that at any time at any time the seller reserve the rights to cancel or postpone the auction until further notice and refunding to the bidder only deposit amount with ought any further claims.

Contacts; you may Contact us through **emmalucas25@yahoo.com** or by calling **+255 717293638.**

**About Reynolds Construction Co. (Nig) Ltd**

Reynolds Construction Co. (Nig) Ltd is recognized for its significant contributions to infrastructure projects across Africa including Nigeria, Kenya and Tanzania. With a robust presence in civil engineering, the company has established a reputation for innovative solutions, quality delivery, and a steadfast commitment to sustainability and compliance. Reynolds Construction Co. (Nig) Ltd continues to lead the industry in setting high standards for excellence and reliability in construction and infrastructure development.

# Watano wafariki dunia kwa kipindupindu, 500 walazwa

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

WATU watano wamepoteza maisha na wengine zaidi ya 500 wamelazwa kwenye kambi maalumu za matibabu wilayani Ikungi, mkoani Singida katika kipindi cha kuanzia mwezi wa saba hadi mwishoni mwa mwezi wa kumi, mwaka huu, baada ya kugundulika kuwa na ugonjwa wa kipindupindu.

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Dk. Emmanuel Kikoti, alisema wagonjwa hao walipatikana katika vijiji vya Kaugeri, Mduguyu pamoja na Ufana na baada ya kutokea kwa mlipuko wa ugonjwa huo serikali wilayani Ikungi, ilichukua hatua za tahadhari kwa kuweka kambi maalumu katika maeneo hayo.

Kwa mujibu wa Dk. Kikoti tangu mlipuko wa ugonjwa huo ulipotokea, kati ya wagonjwa 500 waliopatikana, watano walipoteza maisha na vifo hivyo vilitokea kutokana na wananchi kutokuwa na elimu ya kuwa kambi hizo za matibabu ndizo zitakazowasaidia kupona.

"Kwa upande wa mlipuko wa ugonjwa huu wa kipindupindu ambao tuliweza kuupata katika kipindi cha mwezi wa saba mpaka sasa ambao tunaendelea nao tulianza na Kijiji cha Kaugeri kilichoko Kata ya Mwaru na tukaudhibiti na ukaisha kabisa.

"Lakini baada ya muda tukapata wagonjwa wengine Kata ya Mgungira na tangu ugonjwa huu ulipozuka tumepata wagonjwa 500," alifafanya Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Ikungi.

Aidha, Kaimu Mganga mkuu huyo aliitaja baadhi ya mikakati itakayosaidia kukabiliana na ugonjwa huo kuwa ni pamoja na kusitisha shughuli za uvuvi katika bwawa lililoko kata ya Mgungira, kuwahamasisha wananchi juu ya umuhimu wa kuchimba na kutumia vyoo kwenye kila kaya na umuhimu wa kutunza mazingira katika maeneo yao mbali mbali.

Kaimu Mganga alisema wagonjwa hao hawakufika kwenye kambi mapema kutokana na kutafuta matibabu kwenye maeneo mengine, kwa kujitibu kupitia madawa ya asili na wengine kutofika kwenye kambi za matibabu ya ugonjwa huo.

> **"Tunaendelea kuelimisha kwamba watu waendelee kutumia vyoo kwa sababu kuna asili fulani ya kuchimba vyoo, lakini watu hawatumi kwa sababu ya dhana potofu ya kimila ya kutochangia choo baba na mtoto pamoja na mkwe," alifafanua Mwanga.**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Ally Juma Mwanga, alisema idadi ya wagonjwa wa kipindupindu iliongezeka kutoka sita hadi 500 na kuitaja moja ya sababu ya mlipuko wa ugonjwa huo kuwa ni kutokuwa na vyoo na wenye vyoo kutovitumia.

"Idadi ya wagonjwa iliongezeka kutoka watu sita hadi kufikia watu 500, lakini tulikaa na uongozi mzima wa ngazi ya wilaya kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa huu.

"Gonjwa ni la aibu kwa sababu wananchi wetu kula uchafu kwa sababu jamii ya ukanda huu walio wengi hawana vyoo na hivyo tulikaa tukaweka mikakati na mkakati wa kwanza ilikuwa ni kudhibiti hili gonjwa kwa kufunga bwawa ambalo lina samaki wengi."

Diwani wa Kata ya Mwaru, Iddi Makangale alisisitiza kwamba athari ya kupoteza maisha ya watu haijatokea sana japo kuna watu wawili walipoteza maisha baada ya kupatwa na ugonjwa huo.

"Tunaendelea kuelimisha kwamba watu waendelee kutumia vyoo kwa sababu kuna asili fulani ya kuchimba vyoo, lakini watu hawatumi kwa sababu ya dhana potofu ya kimila ya kutochangia choo baba na mtoto pamoja na mkwe," alifafanua Mwanga.

Tabibu aliyekuwa zamu katika kambi ya wagonjwa iliyoko katika Kijiji cha Ufana, Elisante Ngura, aliweka bayana kwamba walipofika katika kambi hiyo walikuta wagonjwa 11 na baada ya muda walipokea wagonjwa wengine watatu wakawa na jumla ya wagonjwa 14 ambao wameshatibiwa sita na kuruhusiwa na kubaki na wagonjwa wanane ambao wanaendelea vizuri.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz
NFRA

## TANGAZO LA MWALIKO WA KUONYESHA NIA: KUONGEZA UWEZO WA UHIFADHI WA NAFAKA KUPITIA SEKTA BINAFSI

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) unakaribisha maombi kutoka Sekta Binafsi wenye uwezo na sifa zinazostahili kuonesha nia ya kushirikiana na NFRA katika kukabiliana na changamoto za uwezo wa kuhifadhi nafaka. NFRA kwa sasa inaendelea na msimu wa ununuzi wa nafaka kwa mwaka 2024/2025, ambao unajumuisha mahitaji ya akiba ya Taifa, mauzo ya nje, pamoja na mahitaji ya wadau wengine.

Ili kufanikisha lengo hili la kitaifa na kuhakikisha nafaka zilizokusanywa zinahifadhiwa kwa usalama, NFRA inatafuta ushiriki wa sekta binafsi katika kuongeza uwezo wa hifadhi. Aidha uwezo wa sasa haukidhi mahitaji ya NFRA, kuna haja ya haraka ya kutafuta suluhisho la uhifadhi lenye ubunifu na lenye gharama nafuu.

**WIGO WA USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI**

Wadau kutoka sekta binafsi watakaochaguliwa watahitajika kushirikiana na NFRA katika kuongeza uwezo wa ziada wa hifadhi ya nafaka, hasa katika mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Njombe, Morogoro, na Songwe. Wigo wa ushiriki unajumuisha:

i. Kukodisha maghala ya nafaka yanayomilikiwa na sekta binafsi, yenye uwezo wa chini wa kuhifadhi tani 3,000 kwa kila ghala.
ii. Kujenga maghala mapya ya kuhifadhi nafaka kwa mikataba ya upangaji wa muda mrefu ili kukidhi mahitaji ya muda wa kati hadi mrefu, yenye uwezo wa chini wa kuhifadhi tani 3,000 kwa kila ghala.
iii. Kusaidia katika utekelezaji wa mbinu bora za usimamizi wa akiba ili kuboresha utunzaji na uhifadhi wa nafaka.

**VIGEZO VYA USHIRIKI**

Wadau wanaopenda kushiriki lazima waonyeshe:

i. Uzoefu katika usimamizi wa uhifadhi wa nafaka au 'logistics' zinazohusiana.
ii. Uwepo wa maghala yanayokidhi viwango vya NFRA vya usalama wa chakula na ubora.
iii. Utayari wa kushiriki katika jitihada za pamoja za kuboresha usalama wa chakula nchini Tanzania.

**MAELEZO YA UWASILISHAJI**

Wadau kutoka sekta binafsi wanaopenda kushiriki wanatakiwa kuwasilisha nia ndani ya siku kumi na nne (14) tangu tangazo hili litolewe. Uwasilishaji unatakiwa kujumuisha wasifu wa kampuni, maelezo ya uwezo wa hifadhi unaopatikana, eneo la maghala yanayotarajiwa kujengwa, maelezo ya ardhi inayopatikana kwa ajili ya ujenzi, na uzoefu wowote muhimu katika kusimamia miradi mikubwa ya uhifadhi au logistics.

**MAELEZO YA MAWASILIANO**

Tafadhali tuma Nia yako pamoja na maswali yoyote kwa:
Barua pepe: info@nfra.go.tz; hpmu@nfra.go.tz

**Anwani:** **Afisa Mtendaji Mkuu**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula,**
**S.L.P 1050**
**Eneo la Viwanda Kizota, Dodoma, Tanzania.**

Tunatarajia kushirikiana na wadau wenye uwezo na dhamira ya dhati ili kuhakikisha akiba ya nafaka ya NFRA inahifadhiwa kwa mafanikio na kufikia malengo ya kitaifa ya usalama wa chakula.

**Imetolewa na;**
**Dkt. Andrew M. Komba**
**AFISA MTENDAJI MKUU**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz
NFRA

## TANGAZO LA MWALIKO WA KUONYESHA NIA: KUTOA HUDUMA ZA USAFI WA NAFAKA KWA NFRA

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) unakaribisha washiriki kutoka sekta binafsi kuonesha nia ya kutoa huduma za kusafisha kwanzakuweka viwango vya ubora (granding) nafaka, kuchagua nafaka kulingana na rangi, na kuzichambua, Shughuli hizi zitaendeshwa kikamilifu na sekta binafsi katika vituo 110 vya ukusanyaji nafaka nchini Tanzania. Ada ya huduma italipwa na wakulima kwa ajili ya huduma za kusafisha na kuchambua nafaka. Mpango huu unalenga kuhakikisha nafaka bora zinahifadhiwa huku viwango madhubuti vya uchafu vikidhibitiwa.

**WIGO WA KAZI**

i. Uwezo wa Kusafisha Kila Siku: Kuanzia tani 200 hadi tani 350 za mahindi kwa siku katika kituo husika.
ii. Viwango vya Ubora: Ili kukidhi viwango vya NFRA, kiwango cha uchafu hakipaswi kuzidi 0.5% kwa vitu ambavyo sio nafaka 0.25% kwa uchafu usio wa kikaboni, huku punje zilizoharibiwa na wadudu zikibaki chini ya 1.0% na punje zilizovunjika chini ya 2.0%.
iii. Mahitaji ya Kuchagua Rangi: Kwa mahindi meupe, sehemu ya mahindi yenye rangi tofauti (nafaka zilizopoteza rangi) haipaswi kuzidi 0.5%.
iv. Michoro: Washirika wanaopenda wanapaswa kutoa michoro ya ubunifu, ikijumuisha michoro ya mtiririko wa mchakato, mipango ya sakafu, na mipangilio ya urefu ili kuhakikisha upangaji bora wa vifaa na uzalishaji wa juu.
v. Uendeshaji: Kutokana na kusambaa kwa vituo 110 kijiografia, kila eneo lazima liwe na taarifa zake kwa utaratibu ili kukidhi mahitaji maalum ya uendeshaji na kudumisha ubora wa huduma.

**MAHITAJI KWA WASHIRIKI**

Washiriki wenye sifa wanapaswa kuonesha uwezo wa:

i. Kusambaza mashine za kusafisha nafaka na kuchagua rangi zenye uwezo wa kusafisha tani 200-350 za mahindi kwa siku.
ii. Kuhakikisha kuwa mashine zinaendeshwa na kuhudumiwa kikamilifu na sekta binafsi, huku wakizingatia viwango vya ubora wa nafaka, na kuhakikisha wakulima wanapewa taarifa kuhusu ada za huduma husika.
iii. Kutoa mpango wa kina wa usimikaji wa mashine, kuanzisha huduma, na mafunzo kwa wafanyakazi wa NFRA kuhusu uendeshaji na ufuatiliaji wa ubora.

**MAELEZO YA UWASILISHAJI**

Washiriki wanaopenda wanatakiwa kuwasilisha maombi ya Maonyesho ya Nia (EOI) pamoja na wasifu wa kampuni, mbinu zilizopendekezwa, maelezo ya kiufundi ya vifaa, na uzoefu unaofaa katika shughuli za kusafisha nafaka.
Tafadhali tuma Maonyesho ya Nia (EOI) yako ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya tangazo hili kutolewa kwa:

**Anwani:** **Afisa Mtendaji Mkuu**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula,**
**S.L.P 1050**
**Eneo la Viwanda Kizota, Dodoma, Tanzania.**
**Barua pepe: info@nfra.go.tz; hpmu@nfra.go.tz**

Tunatarajia kushirikiana na sekta binafsi zenye uwezo na dhamira ili kuhakikisha shughuli za kusafisha nafaka zinafanyika kwa ufanisi na kuhakikisha nafaka zenye ubora wa juu zinanunuliwa.

Imetolewa na;
Dkt. Andrew M. Komba
**AFISA MTENDAJI MKUU**

## Vijana waibana serikali, wadau wa kilimo

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

JUMUIYA ya viongozi vijana wa mifumo ya chakula mkoani hapa imeitaka serikali na wadau wa kilimo kuwekeza katika kilimo endelevu na cha mijini ili kuongeza upatikanaji wa chakula na lishe nchini.

Micky Lucas kutoka Arusha Food Systems Youth Leaders, alisema kuwa serikali na wadau hao wanapaswa kuongeza uwekezaji katika mbinu za kilimo hicho kwa kuwa utafiti unaonyesha asilimia15 ya chakula kinachozalishwa nchini hupotea kabla ya kufikia walaji.

Ujumbe huo wa vijana kwa madiwani wakiongozwa na Meya wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Maxmillian Iraghe, uliwasilishwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Micky Lucas kutoka Arusha Food Systems Youth Leaders.

"Sehemu kubwa bado inatumia mbinu za zamani na zenye uzalishaji mdogo. Tunataka kuwezeshwa vijana kwenye biashara za chakula na wajasiriamali wa kilimo cha mazao ya chakula kwa sababu vijana ndio mustakabali wa mifumo yetu ya chakula," alisema Lucas.

Alisema vijana bado wanakabiliwa na changamoto za upatikanaji wa ardhi na mitaji na kuwa kikwazo kwa maendeleo yao katika sekta ya kilimo.

Aliiomba serikali kupitia mikopo ya halmashauri itoe kipaumbele kwa biashara za vijana za chakula na ujasiriamali wa kilimo cha mazao ya chakula.

Lucas, alisema vijana hao wanataka serikali ihakikishe inaongeza ushiriki na ushirikishwaji wao na makundi maalumu katika mifumo ya chakula, hasa kwa jamii zilizo pembezoni.

Hoja nyingine aliyoitaja ni viongozi kuwa vinara wa kutokomeza utapiamlo unaotokana na lishe duni na kuboresha mifumo ya chakula.

Ofisa Vijana wa Shirika la Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN), Saddam Khalfan, alisema shirika hilo, kwa kushirikiana na Arusha Food System Youth Leaders, wanaamini Arusha inaweza kuwa jiji safi na lenye usalama wa chakula namba moja nchini.

Alisema wanatoa wito kwa viongozi kuhakikisha masoko ya chakula yanakuwa safi, salama na yenye ufuatiliaji mzuri wa viwango vya usalama wa chakula.

"Hili linaweza kufanikiwa kwa kuwa na mkakati shirikishi, jumuishi na kutungwa kwa kanuni ndogo za usimamizi wa hoja hii ili kuimarisha elimu ya lishe, kumaliza aina zote za utapiamlo.

...ni muhimu kuimarisha elimu ya lishe kwa jamii ili kumaliza aina zote za utapiamlo katika Jiji la Arusha. Vijana tunaamini kuwa elimu bora ya lishe itasaidia watu kufanya maamuzi bora kuhusu chakula na kuongeza hali ya afya na ustawi wa watu," alisema.

Vijana hao wanapigania ukombozi huo baada ya kujengewa uwezo na Mradi wa Nourishing Food Pathway (NFP) unaotekelezwa na GAIN kwa ufadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), Serikali ya Uholanzi, Uingereza na wadau wengine kutoka taasisi binafsi.

# Wanaume wawapigia chapuo wanawake uchaguzi mitaa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

BAADHI ya wanaume mkoani hapa wameanza kuondokana na mfumo dume kwa kuwapa fursa wake zao kujitosa katika kinyang'anyiro cha uchaguzi wa serikali za mitaa nchini Novemba 27, mwaka huu.

Wanaume hao ni wa kata mbili za Manispaa ya Moshi na nne za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi mkoani humo ambazo wanawake wamejitosa sawa kutafuta tiketi ya kuungwa mkono kwenye uchaguzi huo wa wenyeviti wa mitaa, vijiji na vitongoji utakaovishirikisha vyama vingi vya siasa nchini.

Imebainika kuwa wanaume hao wamekubali kubadili mitazamo ya kiitikadi na mfume dume kisha kuwapa nafasi ya wanawake hao kuongoza katika mchakato wa kura za maoni zilizofanyika hivi karibuni katika vyama hivyo vya siasa.

Akizungumza jana katika kikao cha viongozi wanaharakati cha kupeana taarifa za shughuli za mradi huo, Jenifa Kassim, mwanaharakati kutoka Kata ya Kirua Vunjo Kusini, alisema wanashukuru Mungu kwa wanaume hao kubadili tofauti na ilivyokuwa awali.

"Tumeweza kuibadilisha jamii yetu, wanaume sasa wanasikiliza na wamegeuka na wenyewe wamekuwa ni walimu wa kupinga ukatili wa kijinsia, kukemea mfumo dume na kuhamasisha wanawake kuingia katika vyombo vya maamuzi," alisema Jenifa na kuongeza kuwa:

"Wanaume wachache waliopata elimu ya masuala ya ukatili wa kijinsia na usawa wa kijinsia, wamesaidia kuwabadili mitazamo wenzao na wanawake hivi sasa wanaungwa mkono na wanaume kwenye kugombea uongozi kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa, Novemba 27 mwaka huu."

Mwanaharakati Catherine Kusaga, Mkazi wa Kata ya Ngangamfumuni, alisema katika vijiji, mitaa na vitongoji ambako wanawake wameongoza kura za maoni ndani ya vyama hivyo ni maeneo yale yaliyoguswa zaidi na wanaharakati waliojengewa uwezo na Mradi wa Sauti ya Haki unaotekelezwa na Shirika la kiraia la KWIECO, linalofadhiliwa na Women Fund Tanzania Trust (WFT).

Easter Mlay, Mkazi wa Kata ya Mwika Kaskazini, alisema katika eneo lao, wanaume tangu walipopewa elimu, wamewaunga mkono wanawake kwa asilimia 100.

"Ule mfumo dume wa uchagani umeanza kupungua na kutoweka taratibu katika baadhi ya vijiji na vitongoji hasa Mwika Kaskazini. Ni wanawake tu tumejitokeza kwa wingi kwenye midahalo, mahojiano na tutashinda uchaguzi huu," alisema.

Mratibu wa Mradi huo, Veronica Ollomi, alisema kila wanapokutana lazima wapeane majukumu na taarifa ya kilichofanyika ili kufikia malengo waliyopanga kwa kipindi cha miezi mitatu na kitakachoendelea.

"Tunaamini mambo mengi yanafanyika katika ngazi ya maamuzi na kama hatutakuwa na wawakilishi wa wanawake kwenye ngazi za maamuzi ina maana zile ajenda kuhusu wanawake zinakuwa ni ngumu sana kuweza kupata nafasi," alisema.

Kata zinazoguswa na mradi huo ni Pasua na Ngangamfumuni za Manispaa ya Moshi, Mabogini, Mwika Kusini, Mwika Kaskazini na Kirua Vunjo za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.



Mwananchi akipita kando ya barabara kutokana na maji yaliyotuama kujaa kwa sababu ya mvua iliyonyesha juzi katika mtaa wa Kigogo Ilala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wachimbaji madini walia umaskini

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WACHIMBAJI wadogo wa madini mkoani hapa wanakabiliwa na ukosefu wa mitaji na kuendelea kuwa masikini.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (MAREMA), Elisha Mnyawi, akizungumza jana katika mji mdogo wa Mirerani, alisema kuwa ukosefu wa mitaji ni changamoto kubwa ya wachimbaji hao.

Mnyawi, alisema japokuwa mkoa huo una utajiri mkubwa wa madini ya aina mbalimbali, wachimbaji hao wameendelea kuwa maskini kwa kukosa mitaji.

"Nikiambiwa nitaje changamoto kubwa ya wachimbaji madini wa mkoa huu, nitazungumzia kuwa namba moja ni mtaji, namba mbili ni mtaji na namba tatu ni mtaji," alisema Mnyawi.

Alisema wachimbaji hao kutokana na mazingira magumu ya leseni zao, imekuwa vigumu kukopesheka kupitia taasisi za fedha nchini ikiwamo benki.

"Chama chetu cha wachimbaji kimekuwa na ukata mkubwa, kutokuwa na vyanzo vya mapato, zaidi ya kutegemea michango kutoka kwa wahisani na wadau," alisema Mnyawi.

Alisema na viongozi wenzake wamelenga kurekebisha rasimu ya Katiba ya MAREMA ili kufungua miradi ya maendeleo kwa manufaa ya wachimbaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Gracian Makota, aliwatoa hofu wachimbaji hao kwa kusema taasisi za fedha ikiwemo benki, zinatoa mikopo kwa wachimbaji hao na wengine.

Makota, alisema benki zimeona umuhimu wa kuwapa mikopo na kuwataka wajipange ili waweze kunufuka na kufanya shughuli za uchimbaji ipasavyo.


"Tena na mwenyekiti mtanashati mwenye mwonekano wa kiungwana anayevaa suti bila kutoka jasho, ninaamini atawavusha na kuwapeleka eneo zuri wachimbaji," alisema Makota.

Mwenyekiti Mstaafu wa MAREMA, Justine Nyari, alisema ana uhakika chama hicho kitapiga hatua kwa kuwa kiongozi wake wa sasa, Elisha Mnyawi ni kijana mwenye maono, dira na mtazamo wenye kuona mbali.

"Sisi tumeifikisha MAREMA hapa ilipo na kupitia uongozi wa Mnyawi nina uhakika mtapiga hatua kubwa na kuendeleza mazuri tuliyoyafanya kwa kuwafikisha wachimbaji mbali zaidi," alisema Nyari.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Money Yusuf, alisema wachimbaji madini wanapaswa kuendelea kushirikiana na kuanzisha mfuko utakaowainua na kufikia malengo waliyojiwekea.

"Mkiweka mitaji kwenye mfuko wenu mtaweza kukopesheka kwenye mabenki kupitia fedha zetu na kufanya shughuli zenu ikiwamo kununua mitambo ya uchimbaji," alisema.





# CHADEMA, CCM wapeana angalizo wakirejesha fomu

**Na Samson Chacha,** TARIME

WAGOMBEA wa nafasi mbalimbali katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) pamoja na Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Tarime, mkoani Mara wamekamilisha ngwe ya urejeshwaji fomu huku wakiwaomba wananchi kushiriki ipasavyo katika kupiga kura ili kuwapata viongozi wa kuwatumikia.

Walitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki ikiwa ni ukomo wa urejeshwaji fomu katika maeneo yote nchini, Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Tarime, Mwita Sasi, akiwataka kufanya kampeni za kistaarabu na kuepuka vurugu zinazoweza kujitokeza wakati wa kampeni zitakapoanza Novemba 20, mwezi huu.

"Tumeweka wagombea wetu katika Halmashauri ya Tarime Vijijini yenye vitongoji 500, vijji 88 na kata 26 ambako tuna wagombea zaidi ya 400 na tunaahidi kuhamasishwa wananchi na wanachama wetu kushiriki kikamilifu katika hatua zote," alisema Sasi.

Alitaja kata zenye ushindani mkali na zenye wapigakura wengi kuwa ni pamoja na Sirari na kuwa kote wamewekwa wagombea, wakiwamo wagombea ambao wamewahi kushika nafasi za udiwani.

Wagombea kupitia CCM nao walirejesha fomu katika ofisi za watendaji kata huku wakisindikizwa na Madiwani Amos Sagara na Victoria Mapesa.

Madiwani hao waliwataka wanachama wao kutokufanya vurugu za aina yoyote pindi kampeni zitakaporuhusiwa kuanza na kuomba uungwaji mkono, ili kumalizia miradi iliyoanzishwa, ikiwamo ya maji, elimu, barabara na afya.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Chikole wakipatiwa uji wa lishe bora na walimu wao, siku ya maadhimisho ya lishe yalifanyika Kata ya Msalato Dodoma jana. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Vijana wakumbushana shamba kuepuka utegemezi wa kamari

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BAADHI ya vijana waliojikita katika shughuli za kilimo kutoka maeneo mbalimbali wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, wamewataka wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu kuacha kubweteka nyumbani wakisubiri kuajiriwa na kuendekeza michezo ya kubeti 'kamali' bali wajikite katika kilimo kujiinua kiuchumi zaidi ya ajira wanazozisubiri.

Wametoa wito huo kwa nyakati tofauti wakizungumza na Nipashe hali ya kilimo na ushiriki wa vijana katika shughuli hiyo ambayo vijana wengi wamekuwa wakitajwa kuikimbia.

Mkazi wa Kijiji na Kata ya Nyandekwa, George Masatu, alisema kila mwaka amekuwa akilima zaidi ya hekari sita za mazao ya chakula na biashara na amekuwa akinufaika kwa kuuza mpunga na alizeti na fedha anazozipata anafanya maendeleo kwenye familia yake.

Alisema msimu wa kilimo 2018/19 alikuwa miongoni mwa vijana walioweza kunufaika na pembejeo zilizokuwa zinatolewa bure na halmashauri na ndizo zilizomfanya kuona umuhimu wa kilimo, na msimu huu atalima zaidi kwani kilimo kimekuwa kikimpatia fedha nyingi kulinganisha na alivyokuwa akicheza michezo ya kubahatisha.

Magreth Juma Mkazi wa Kilago alisema idadi kubwa ya vijana wanaotarajiwa kuinua jamii kwa kutumia elimu waliyoipata kuanzia darasa la saba hadi chuo kikuu bado wamewekа kipaumbele katika michezo ya kubahatisha 'kamali' pamoja na kusubiri ajira za serikali.

"Wanaotoka vijijini tuko 'busy' shambani kutafuta mali ushauri wangu kwao waache kusubiri ajira na kujiendekeza na michezo ya kubeti sambamba na serikali ifanye mikutano kila kata kuwaelimisha vijana umuhimu wa kilimo," alisema Magreth.

Alisema msimu uliopita kulikuwa na mvua chache kulinganisha na misimu mingine, lakini aliweza kupanda mazao yanayostahimili ukame na alipata mazao ya kula na familia, na sasa anajiandaa kuandaa mashamba kwa ajili ya kilimo cha mpunga na pamba.

Akizungumza na Nipashe kuhusu wanavyoshiriki kuinua vijana waliojikita katika kilimo wilayani hapa, Katibu wa Mbunge wa Jimbo la Kahama, Abdul Mpei alisema ofisi ya jimbo hilo imetoa majembe 7,115 bure kwa vijana kila kata ili kuhakikisha wanajikita kwenye kilimo chenye tija.

Mpei alisema kati ya majembe hayo yaliyotolewa 7,000 yalikuwa ya kutumia mikono na majembe 115 ya kutumia au kuvutwa na ng'ombe wanaotumika kwenye kilimo shambani.

Alisema wamekuwa wakishirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Idara ya Kilimo na kuwa mwaka 2024/225 halmashauri hiyo imetenga zaidi ya Sh. milioni 50 za kununua pembejeo na viwatilifu kwa ajili ya kilimo cha pamba na kuwataka vijana kujitokeza kwa wingi kuchangamkia fursa hiyo.

## Wataka udhibiti vipimo vya sukari visivyo sahihi

**Na Remmy Moka,** MWANZA

BAADHI ya wananchi mkoani Mwanza wameomba serikali kuja na mkakati wa udhibiti wa vipimo visivyo na usahihi katika upimaji sukari, ili kuleta uwiano sawa wa ujazo na gharama ya bidhaa hiyo.

Wananchi hao, akiwamo Rehema Hamidu, mkazi wa Kiroleri, walitoa ombi hilo kwa nyakati tofauti na kueleza kuwa wamekuwa wanakabiliwa na changamoto zinazohusiana na sukari ya kupima, ambayo mara nyingi hupimwa kwa mizani inayotumiwa pia kupima bidhaa nyingine kama vile maharage na unga.

"Katika mizani hii imekuwa ikikosa usahihi na kutupa wasiwasi juu ya kiwango tunachochukua kutokana na kuwa kidogo kulinganisha na kiwango unachonunua mfano unanunua kilo moja, lakini ni kama robo tatu hivyo ni bora uwepo udhibiti wa vipimo vya moja kwa moja kutoka viwandani unaojulikana," alisema Rehema.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Mkurugenzi wa Biashara wa Kampuni ya Sukari Kilombero, Fimbo Butallah, alisema tayari kampuni hiyo imeanza utaratibu wa kuwa na vifungashio vya moja kwa moja ambavyo vimedhibitiwa.

"Kupitia chapa yetu ya Bwana Sukari, tumezindua sukari yenye vifungashio jijini Mwanza ambayo itaweka unafuu wa bei, usafi, afya ya mlaji na urahisi wa upatikanaji bidhaa hiyo kulinganishwa na sukari za kupima," alisema Butallah.

Alisema hatua hiyo inatarajia kumaliza malalamiko yaliyopo juu ya usahihi wa vipimo, usafi na gharama nafuu, kwani wateja walionekana kupunguza uaminifu kwenye sukari za kupima, huku wakilaumu mizani isiyo na uaminifu kwa kupokea kiasi kidogo cha sukari kulingana na walicholipia.

Katibu Tawala Wilaya ya Ilemela, Mariam Msengi, akizungumza juzi wakati wa uzinduzi wa sukari iliyofungashwa kutoka kampuni hiyo, alisema itakuwa na mchango mkubwa wa kuboresha maisha ya wakazi wa Mwanza na Kanda ya Ziwa na kuleta usahihi katika vipimo.

## Madiwani waijia juu TANESCO kwa kutosambaza umeme vijijini

**Na Timothy Itembe,** RORYA

MADIWANI wa Halmashauri ya Rorya, mkoani Mara wamelikosoa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wilayani hapa kwa kushindwa kufikisha umeme kwenye baadhi ya vitongoji na kusababisha wananchi kukosa huduma hiyo.

Akizungumza katika kikao cha baraza lao, Diwani wa Nyancha, Roja Okuku alisema kipindi hiki si cha wananchi kukaa gizani na shirika hilo linarudisha nyuma maendeleo ya wananchi.

Alihoji vigezo vinavyotumiwa na shirika hilo kuwafikishia umeme wananchi, akitoa mfano wa kijiji cha Sota, ambako kuna wateja wengi wanaohitaji huduma bila mafanikio.

Diwani wa Komuge, Wilsoni Marwa, alisema kuna vitongoji vingi havijapatiwa umeme, akitaja umuhimu wa huduma hiyo kwa taasisi kama shule.

Akijibu hoja hizo, Kaimu Meneja wa TANESCO Wilaya Rorya, Budeba Kihanda, alikiri kuwapo uhitaji mkubwa wa huduma hiyo na kuwa mkandarasi tayari ametia saini mikataba na utekelezaji mradi huo unatarajiwa kuanza ndani ya mwaka huu wa fedha (2024/25).



Ukurasa 12

**UDSM yaja na kituo cha jinsia, wenye ulemavu kuongeza elimu kiushirikishi**



Ukurasa 13

Mawasiliano ya kielektroniki yanavyoibua shangwe serikalini



Ukurasa 14

**Stadi za maisha kwa wasichana zinavyowapa ujasiri mabinti shuleni**

Nipashe

TESA

Jumanne Novemba 5, 2024

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

ELIMU

NA MAULID MMBAGA

# Ni zama za mabadiliko Wamasai wanapogeuka wakulima mahiri

NI kwa nadra kumkuta Mmasai njiani na jembe begani akielekea shambani. Tena si kawaida kuwaona wameinama wanalima, japo kuna baadhi ya jamii za Wamasai wanaojulikana kama Wakwavi ambao hufuga na kwa kiasi wanalima.

Leo, zama zimebadilika baada ya wadau wa kilimo kuibua mikakati ya kuhamasisha na kubadilisha jamii hiyo na sasa inaingia mashambani kuzalisha mazao.

Ni jitihada ambazo Taasisi ya Uendeshaji wa Mifumo ya Masoko ya Kilimo (AMDT), imekuwa ikizifanya kwa miaka kadhaa ikiwamo kutoa elimu na kujenga miundombinu ya umwagiliaji ambazo zimebadili mtazamo wa wafugaji hao na kujikita katika uzalishaji.



Mkulima Mathayo Olonyoke, akiwa kazini kwenye shamba alilootesha mikunde. **PICHA: MAULID MMBAGA**

Ofisa Kilimo wa Kata ya Ondonyongijape wilayani Simanjiro mkoani Manyara, ambako idadi kubwa ya wananchi ni Wamasai, Jenifa Mbuya, anasema eneo hilo takribani asilimia 99 wakazi wake ni wakulima.

Anasema wale walioanza kulima mwanzoni wamekuwa sehemu ya kuwashawishi wanaotegemea ufugaji pekee kubadilika, akieleza kuwa wakulima wamekua na chakula cha uhakika na familia hazina njaa.

"Waliokuwa wa kwanza kulima akipata changamoto anauza gunia la maharage na kujihudumia, hauzi mifugo hivyo aliongeza ng'ombe huku ikitatua matatizo mengine na kuona kuwa kilimo ni tija.

"Waliokuwa wanasema Wamasai hawalimi sio wa Simanjiro. Leo asilimia kubwa wameingia kwenye kilimo, kwa kushirikiana na AMDT tuliweka mashamba darasa wamependa na kujiendeleza," anasema Jenifa.

Kwa takwimu za awali inaelezwa kuwa jitihada hizo zimekuwa na matokeo chanya kiasi cha kuwafanya wafugaji kuona kwamba kilimo na ufugaji vyote vina thamani sawa.

Mathayo Olonyoke, mkazi wa Kijiji cha Orkirung'urung'u, Simanjiro, mfugaji wa jamii ya Kimaasai, anasema alianza kulima baada ya kuibuka changamoto za mabadiliko ya tabianchi ziliathiri ufugaji.

Anasema wakiwa katika harakati za kutafuta mbadala wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi AMDT iliwapatia elimu ya namna ya kufanya kilimo cha kisasa.

Anabainisha kuwa ni miaka 20 sasa tangu aanze kulima na kwamba baada ya kupatiwa elimu na taasisi hiyo ikishirikiana na kampuni ya mbolea ya Beula kuhusu kilimo cha umwagiliaji wa matone, amezidi kupata mafanikio yanayochochea hamasa kwa jamii hiyo.

"Nawaambia wafugaji na Wamasai wenzangu kwamba kilimo ni kizuri na kinasaidia kupiga hatua kimaisha. Ingawa kuna changamoto lakini hata kwenye ufugaji ziko pia, lakini kutokana na hatua niliyoipiga hata nikiwaambia wafugaji tulime inakuwa rahisi kunielewa kwasababu kila kitu wanakiona," anasema Olonyoke.

Anasema kupitia mradi wa maono ya mabadiliko kwenye mazao na udongo (VACS), unaoendeshwa na AMDT, wananufaika na mbegu bora na kuhamasishwa kulima choroko na kunde zinazovumilia ukame.

Anafafanua kuwa kilimo hicho kimekuwa na uhakika wa chakula muda wote, akieleza kwamba kabla hawajafikiwa na mradi huo wa umwagiliaji hawakuwahi kupata mboga za maharage katikati ya msimu au kwenye kiangazi.

"Manufaa tunayo kwasababu tukitaka mboga leo tunapata kwa wakati, binafsi najisikia vizuri na ninafikiri wafugaji wenzangu wanatamani ninachokifanya na kila siku wananipongeza na wengi wanaahidi kujiunga na mimi," anasema Olonyoke.

Aidha, anaomba wadau mbalimbali kuwashika mkono kwa kuwachimbia visima zaidi ili waongeze ukubwa wa mashamba kwasababu wana maeneo mengi lakini wanashindwa kuyapanua kutokana na uhaba wa maji.

**KUBADILI MTAZAMO**

Kuhusu migogoro ya wafugaji na wakulima Olonyoke anaeleza kuwa wanakijiji wamewekeana miongozo kwa kushirikiana na ofisa kilimo wa eneo hilo, akieleza kwa sasa imefika hatua wanaona kuwa kilimo ni bora kama ufugaji na hawataki shughuli yoyote iiathiri nyingine.

Anasema wameshapiga vita na kukemea masuala ya kudhuru ng'ombe na kwamba inapotokea mifugo imeharibu mazao, wanataka ofisa kilimo atathimini shamba kisha ichukuliwe hatua haraka mkulima alipwe fidia.

Hata hivyo, anaeleza kuwa kilimo cha kisasa cha umwagiliaji ambacho amekuwa akijihusisha nacho kwa zaidi ya miaka 20, kimempatia mafanikio mengi ikiwamo kuchochea hali yake ya kiuchumi, uhakika wa chakula na kusomesha watoto wake ambao wako chuo kikuu.

Anasema ujuzi na zana ya kilimo anavirithisha kwa watoto wake, akieleza kuwa hakuna mtoto katika familia zao ambaye hajui kulima.

**INAENDELEA UK.12**

ELIMU

NA GRACE MWAKALINGA

# UDSM yaja na kituo cha jinsia, wenye ulemavu kuongeza elimu kiushirikishi

KATIKA juhudi za kuwafikia na kuwahudumia wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha masuala ya usawa wa kijinsia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kinajenga kituo maalumu kwa ajili ya wanafunzi, wafanyakazi na wageni.

Kituo hicho kitashughulikia masuala mbalimbali yanayohusiana na jinsia na ulemavu, kutoa msaada wa kisaikolojia, vifaa saidizi na elimu kuhusu haki za binadamu na ukatili wa kijinsia ni mradi unaongeza pia miundombinu rafiki kwa wenye mahitaji maalumu.

Kujenga kituo hicho kitakachotoa huduma kwa wakati mmoja yaani 'one-stop center' ni juhudi za UDSM kuimarisha elimu jumuishi, kuweka mazingira salama yanayowashirikisha wote na kutoa kipaumbele zaidi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Kituo hicho, kinajengwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (WB) ambayo inazisaidia taasisi 23 za elimu ya juu, kujenga miundombinu ya elimu na huduma muhimu kwa ajili ya wanafunzi kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).

Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Jinsia UDSM, Dk. Lulu Mahai, anaiambia Nipashe kuwa dhamira ya kituo hicho ni kuhudumia kwa ukarimu, ukaribu na ufanisi wanafunzi na wadau wenye ulemavu wa aina mbalimbali kwa kuwapatia huduma kulingana na mahitaji yao maalum, ikiwamo usaidizi wa kijamii na kitaaluma.

"Kituo hiki kitatoa nafasi kwa wanafunzi wote wenye ulemavu, aidha na wenye kuhitaji msaada wa kisaikolojia, na huduma nyingine kwa wanafunzi wa kawaida ili kukabiliana na ukatili wa kijinsia, tutahakikisha wanapata msaada unaostahili ili kuimarisha elimu na kufanikisha malengo yao ya kitaaluma, kituo hiki ni sehemu muhimu ya mpango wa chuo kuhakikisha ushirikishwaji wa makundi yote katika elimu ya juu," anasema Dk. Lulu.



Wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanahitaji mazingira na miundombinu rafiki kwenye elimu. **PICHA: MTANDAO**

Anaongeza kuwa kituo hicho kitakuwa na dawati maalum la kushughulikia changamoto zinazohusiana na jinsia, ili kuhakikisha mazingira yasiyo na unyanyasaji wa kijinsia na kuweka mbele haki na usawa wa kijinsia, anasema chuo kimejitolea kuhakikisha kuwa mahali salama dhidi ya unyanyasaji wa aina yoyote.

Anasema chuo kilianza kupokea watu wenye ulemavu mwaka 1978 wakiwa wanaume, anasema waliendelea kupokea na hadi sasa wanao zaidi ya 20.

### HISIA ZA WALENGWA

Mwakilishi wa WB, Profesa Roberta Malee, anaipongeza UDSM kwa kujenga kituo cha kwanza cha aina hiyo nchini, akisema ni jambo la kimapinduzi siyo kwa Tanzania, bali Afrika pia.

"Tunafurahi kuona mnafanya mapinduzi makubwa kwenye elimu jumuishi tuna matumaini mradi huu utaboresha maisha ya wanafunzi wote kwa kutoa nafasi za kipekee za kujifunza na kukua katika mazingira yanayowajali." Anasema Prof. Roberta.

Erick Nyanda, mwanafunzi mwenye ulemavu chuoni hapo, anaelezea matumaini makubwa kuhusu mradi huo akisema kituo hicho kitakuwa kiunganishi cha wanafunzi wenye ulemavu na wale wasio nao.

Anasema kitawawezesha wote kubadilishana mawazo, kushiriki michezo na mazoezi mbalimbali ya viungo, jambo litakalokuza umoja na ushirikiano miongoni mwao.

"Tutaweza kupata msaada wa moja kwa moja kwa mahitaji yetu maalum, ikiwamo ushauri wa kisaikolojia na vifaa vya kisasa vya teknolojia vya kujifunza," anasema Erick.

Mashukura Kabwogi, mtafsiri wa lugha za alama UDSM, anasema kituo hicho kitawasaidia wanafunzi wenye ulemavu kupata huduma stahiki na kujifunza bila vizuizi. Mradi wa ujenzi wa kituo hiki ni sehemu ya Mpango wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), mpango wa miaka mitano unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kuimarisha elimu ya juu.

Dk. Liberato Haule, Naibu Mratibu wa HEET UDSM, anasema utagharimu Dola za Marekani milioni 47.5 (sawa na shilingi bilioni 109) kuboresha miundombinu ya elimu, ujenzi wa madarasa, mabweni, maabara, na vituo vingine katika kampasi mpya za chuo hicho zilizopo mikoa ya Kagera, Lindi na Mtwara.

Aidha, anasema katika kuboresha utoaji wa elimu, wametengeneza mitaala 98 ambayo ipo kwenye hatua za mwisho za kupata ithibati kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania(TCU) ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

Anaongeza kuwa tayari walimu 38 wamepata mafunzo ya kujifunza teknolojia mbalimbali viwandani na pia wataalamu 31 kutoka sekta mbalimbali wameshiriki kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa UDSM.

Anasema kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimefanya juhudi mbalimbali kutekeleza sera, sheria, na miongozo inayohusiana na haki za watu wenye ulemavu, hususan katika elimu ya juu.

UDSM imetekeleza, Sera ya Taifa ya Watu Wenye Ulemavu (2004), ambayo inasisitiza umuhimu wa kuwezesha wenye ulemavu kujumuishwa katika jamii, anaongza Dk. Haule.

Chuo kimeandaa mikakati inayolenga kuboresha mazingira ya kujifunzia, ikiwa ni pamoja na kufanya mabadiliko katika mitaala na kutoa vifaa vya kusaidia wanafunzi wenye ulemavu, anasema.

Naibu Mratibu wa HEET UDSM, anasema chuo kimezingatia pia Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (2010), ambayo inalinda haki zao katika mazingira ya elimu.

Kadhalika, anasema kimetimiza matakwa ya Katiba ya Tanzania (1977) inayotaka kuwapo misingi ya haki za binadamu, ikiwamo haki za watu wenye ulemavu, na inasisitiza umuhimu wa usawa katika kupata elimu na huduma nyingine.

Akizungumzia mradi wa HEET na mustakabali wa elimu Tanzania, anasema unatarajiwa kuwa na matokeo makubwa kwenye elimu ya juu kwa kuboresha miundombinu, vifaa na mitalaa ya kisasa ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata elimu inayolingana na mahitaji ya kiuchumi ya sasa na ya baadaye.

Aidha, Dk. Haule anasema mradi huo pia unalenga kuajiri walimu, watafiti, na wasimamizi wenye ujuzi na kufundisha kwa viwango vya kimataifa.

## Ni zama za mabadiliko Wamasai wanapogeuka wakulima mahiri

INATOKA UK.11

"Ninavyo vifaa mbalimbali kama trekta na vijana wangu wanaoendesha, wanalima wanaotesha wenyewe, wanapalilia na wanafanya kila kitu, hivyo inatosha kusema kwamba kwa sasa kwenye kilimo tumebobea, tunalima na kufundisha wengine," anasema Olonyoke.

Baraka Mathayo, ni mtoto wa Olonyoke, anasema amemuona mzazi wake akijihusisha na kilimo kwa muda mrefu, na ndicho kilichomsomesha kuanzia ngazi ya msingi hadi elimu ya juu akiwa mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Elimu DUCE.

Anamtaja mzazi wake kuwa ni mkulima mahiri anayeshirikiana na wataalamu wa kilimo kama AMDT na Beula katika kumwongezea mbinu mbalimbali za kitaalamu na kulima kwa tija.

"Katika mradi huu wa umwagiliaji naona kuna mafanikio makubwa kwasababu ukiangalia shamba linapendeza muda wote, tunapata mboga na chakula kwa wakati wote hatuhitaji kununua hata maisha tunayaona ni mazuri.

Anaongeza: "Kutokana na elimu yangu, nitapambana kuendelea kuelimisha jamii yetu ya Kimasai kuhusiana na kilimo kwasababu ndicho kilichompa mzazi wangu pembejeo kama trekta, nyumba, kuongeza miundombinu ya kilimo, kununua ardhi, pamoja na kutusomesha na wadogo zangu," anasema Mathayo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Orkirung'urung'u, Noa Moringe, anasema miezi ya Septemba na Oktoba afya ya mifugo inadhoofika, wakati huo huo thamani ya mazao ikipanda, na kwamba hiyo ni moja ya sababu iliyowashawishi wafugaji kujihusisha na kilimo.

ELIMU
NA ROMANA MALLYA

# Mawasiliano ya kielektroniki yanavyoibua shangwe serikalini

KWANINI tusijenge mfumo wa baruapepe serikalini ili kila mtumishi wa umma afanye mawasiliano ya kiofisi kupitia utaratibu huo?

Ndilo swali lililoifanya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) miaka 10 iliyopita, kusanifu na kujenga mfumo wa baruapepe wa serikali (Government Mailing System (GMS) mwaka 2014.

Wakati huo ukiitwa Wakala wa Serikali Mtandao - eGA), Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict Ndomba, anasema.

Anongeza kuwa dhamira ya ujenzi wa mfumo huo ni kurahisisha mawasiliano kati ya taasisi za umma na wadau wake, kuimarisha usalama wa taarifa za serikali.

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni nyenzo muhimu na wezeshi katika utendaji kazi wa shughuli mbalimbali, zikiwamo za kijamii na kiuchumi pamoja na utoaji wa huduma kwa umma, anasema Ndomba.

Anabainisha kuwa, kabla ya maendeleo ya sayansi na teknolojia, mawasiliano rasmi ya kiofisi baina ya taasisi na wadau wake yalikuwa ni barua na majalada, yote yakitumia karatasi.

Ilikuwa ni gharama kubwa na mchakato wenye kuchukua muda mrefu, hivyo kupunguza tija na ufanisi katika utendaji kazi na utoaji huduma kwa umma.

Hivyo, katika jitihada za kutafuta suluhisho la changamoto hizo na kutokana na fursa ya maendeleo ya teknolojia, e-GA ilisanifu na kuanza ujenzi wa mfumo huo wa baruapepe serikalini.

"Lengo la hatua hii ilikuwa ni kuboresha huduma ya mawasiliano baina ya taasisi za umma na wadau wake," anasema Ndomba.

Anakiri kuwa GMS imerahisisha mawasiliano katika taasisi za umma na wadau wake pamoja na kuwawezesha viongozi na watendaji kufanya uamuzi kwa wakati.

Anafafanua kuwa kabla ya kuwapo kwa mfumo huo, baadhi ya taasisi za serikali zilikuwa zinatumia mifumo ya baruapepe binafsi iliyotengenezwa na makandarasi.

Wengine walitumia baruapepe za muda mfupi kutoka kwa watoa huduma kama vile Yahoo na Gmail kwa ajili ya kubadilishana taarifa na nyaraka mbalimbali.

"Mifumo ya baruapepe ya aina hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali za kiusalama, kwani utunzwaji wa taarifa hizo haukuwa wazi kwa serikali kwa kuwa, hakukuwa na makubaliano yoyote kuhusu usalama wa taarifa kati ya serikali na watoa huduma wanaomiliki mifumo hii," anafafanua Ndomba.



Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Benedict Ndomba. **PICHA: MTANDAO**

Anabainisha kuwa, gharama za ununuzi na uendeshaji wa mifumo hiyo zilikuwa kubwa na ufanisi ulikuwa mdogo.

Anasema matumizi ya mfumo wa GMS sio tu umeokoa kiasi kikubwa cha fedha serikalini, bali pia umehakikisha usalama wa taarifa zake na uhakika wa upatikanaji wa huduma ya mawasiliano kwa njia ya baruapepe katika taasisi za umma.

"Katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanza kutumika kwa mfumo wa GMS, mawasiliano kwa njia ya baruapepe kati ya taasisi za umma yamekuwa ya uhakika na salama zaidi.

"Ikiwa ni pamoja na kuziwezesha taasisi zote za umma kufanya mawasiliano kwa njia ya baruapepe kwa kutumia kikoa (domain) cha ofisi husika hali inayowezesha utambulisho wa taasisi inayohusika," anasema Ndomba.

Anaongeza kuwa, moja ya majukumu ya mamlaka ni kutengeneza miundombinu na mifumo shirikishi kwa ajili ya matumizi ya taasisi za umma kwa lengo la kupunguza kurudufu mifumo ya TEHAMA.

Hivyo, anasema usanifu, ujenzi na matumizi ya mfumo huo wa GMS, ambao sasa unatumiwa na taasisi zote za serikali, umeondoa utitiri wa mifumo ya baruapepe iliyokuwa ikitumiwa katika taasisi mbalimbali za umma.

Aidha, umepunguza gharama za uendeshaji kwa serikali kwa kila taasisi kununua na kuendesha mfumo wake wa baruapepe.

Ndomba anasema hadi sasa jumla ya taasisi na vituo vya kutolea huduma zaidi ya 700 zinatumia mfumo wa GMS zikiwamo wizara na idara zinazojitegemea, mashirika ya umma, taasisi za umma, majiji, manispaa, mamlaka na wakala za serikali pamoja na halmashauri za wilaya.

"Mfumo wa GMS hufanyiwa maboresho mara kwa mara kadri mabadiliko ya teknolojia yanavyojitokeza ili kudhibiti usalama wa mfumo pamoja na kukidhi mahitaji ya watumiaji.

"Kwa kuwa, kadri mabadiliko ya teknolojia yanavyojitokeza, pia mahitaji ya watumiaji katika mfumo huongezeka na wakati mwingine, inatupasa kuongeza mambo mapya ili kukidhi mahitaji ya watumiaji," anasisitiza Ndomba.

Kadhalika, anasema kuwapo kwa mfumo wa baruapepe wa serikali kumewezesha taasisi zote za umma kuwa na baruapepe zenye kikoa cha jina la taasisi husika kwa watumishi wake wote bila kujali taasisi ina uwezo kifedha au lah.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Wahasibu Tanzania (NBAA) Pius Maneno, anasema, mfumo wa GMS umerahisisha kutuma na kupokea barua ndani ya taasisi za umma.

Anasema awali kutuma barua za kawaida kulitumia muda mrefu hadi kufika ofisi iliyokusudiwa na muda mwingine barua hiyo hufika kwa kuchelewa na kuathiri utoaji huduma.

"Sasa hivi kupitia GMS kila taasisi imetengenezewa akaunti maalumu kwa ajili ya kutuma barua, hapa NBAA tunatumia barua@nbaa.go.tz na baada tu ya kubonyeza kitufe cha kutuma, barua inakuwa imemfikia mhusika bila kuchelewa," anasema Maneno.

Ofisa TEHAMA Mwandamizi Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Salumu Ally Kulindwa, anaipongeza e-GA kwa kutimiza miaka 10 ya matumizi ya mfumo wa GMS, na kuishauri e-GA kuimarisha ushirikiano zaidi kati yake na taasisi nyingine za umma ikiwamo COSTECH.

"Katika miaka 10 ya matumizi ya mfumo wa GMS, COSTECH tunajivunia sana mfumo huu kwani e-GA imekuwa ikitoa ushirikiano wa haraka pale tunapopata changamoto yoyote katika matumizi ya mfumo huu au hata mfumo mwingine, e-GA hutatua changamoto hizo na kutoa mrejesho kwa wakati," anasema Salum.

Ofisa Uhusiano na Mawasiliano Mwandamizi wa Bodi ya Wahasibu Tanzania (NBAA), Margreth Kageya, anasema mfumo wa GMS umerahisisha utumaji na upokeaji wa taarifa za serikali kwa taasisi za umma.

Dk. Adolar Duwe, Ofisa Utumishi Mkuu kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu Bohari ya Dawa (MSD) anasema, anasema awali gharama za uendeshaji wa mifumo ya baruapepe katika taasisi za umma zilikuwa kubwa.

Anaeleza kuwa changamoto yoyote ya mfumo ilikuwa ikitokea, ilibidi kumlipa mkandarasi kuleta mtaalamu aliyejenga mfumo huo ili kutatua changamoto husika.

Mkurugenzi wa Usimamizi wa Huduma za TEHAMA wa e-GA, Ricco Boma, anasema mamlaka hutoa mafunzo ya usimamizi wa mfumo huo ili kuwajengea uwezo maofisa wa vitengo vya TEHAMA serikalini, waweze kusimamia ipasavyo uendeshaji wa mfumo huo kwa ufanisi zaidi.

Meneja wa Huduma za Sheria wa e-GA Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi (SACP) Rafael Rutahiwa, anatoa wito kwa watumishi wa taasisi za umma, kutumia mfumo wa GMS, kila wanapofanya mawasiliano ya serikali, kwani kutokufanya hivyo ni uvunjifu wa Sheria ya Serikali Mtandao ya Namba 10 ya Mwaka 2019.

Katika kuadhimisha miaka 10 ya matumizi ya GMS, faida nyingi zimepatikana zikiwamo kuongezaka kwa tija na ufanisi wa huduma ya mawasiliano serikalini, pamoja na kuimarika kwa usalama wa taarifa za serikali.

> Mfumo wa GMS hufanyiwa maboresho mara kwa mara kadri mabadiliko ya teknolojia yanavyojitokeza ili kudhibiti usalama wa mfumo pamoja na kukidhi mahitaji ya watumiaji.

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA

# Stadi za maisha kwa wasichana zinavyowapa ujasiri mabinti shuleni

ELIMU kwa msichana ni kila kitu, ni uwekezaji ambao taifa linavuna mama, mke na mzalendo bora aliyeelimika na mshiriki wa maendeleo endelevu.

Pia elimu hiyo ni nyenzo inayowezesha msichana kujitegemea kiuchumi, kuchangia maendeleo ya jamii yake, kufanya maamuzi bora kuhusu afya yake, ndicho wanachosema Shirika la Room to Read.

Taasisi hiyo inayotekeleza mradi wa elimu kwa msichana katika mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es salam na Morogoro, ni katika juhudi hizo imewafikia wasichana 19,000 wakinufaika na elimu hiyo.

Katika mradi huo watoto wa kike wamenufaika na elimu ya stadi za maisha ambayo kwa asilimia kubwa ikiwawezesha kujiamini na kuanzisha miradi midogo ya kuwaingizia kipato.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Room to Read, Agripina Kadama, anasema mitaala ya elimu ya stadi za maisha imetoa mwanga na kwamba ni wakati wa kuendelea kushirikiana na wadau, serikali na wazazi na walezi kuwezesha stadi za maisha kuwa msaada kwa watoto wa kike.

Agripina anaiambia Nipashe kuwa katika mradi huo wasichana 19,000 wa mikoa ya Morogoro, Tanga, Pwani na Dar es Salaam wamefikiwa.

"Watoto wakipatiwa stadi za maisha zinaokoa taifa la kesho vivyo hivyo vizazi vijavyo vya mtoto wa kike vinatakiwa kupewa fursa hiyo," anasema.

Anaipongeza serikali kwa ujenzi wa mabweni kwenye baadhi ya shule kumlinda mtoto wa kike kwa kumuokoa na vishawishi vya njiani anapoelekea shuleni, kurejea nyumbani na kushirikiana na jamii inayomzunguka.

Anasema Room to Read inaamini kuwa msichana aliyeelimika analea watoto wenye afya na wasomi na hivyo kuvunja mzunguko wa umaskini, ujinga na maradhi, utapiamlo na udumavu.

Kadhalika wanawake walioelimika wanachangia katika kukuza uchumi kwa kufanya kazi katika sekta mbalimbali. Elimu hiyo inawajengea uwezo wa kuanzisha biashara na hivyo kujikwamua kiuchumi, wanawake walioelimika wanajua umuhimu wa afya na hivyo kutunza afya zao na za familia. Pia wanakuwa na uwezo wa kupanga familia zao na hivyo kuchagua idadi ya watoto wanayotaka kuwa nao.



Kubuni mitindo na kushona ni moja ya stadi za kazi wanazojifunza mabinti shuleni. **PICHA: MTANDAO**

> Watoto wakipatiwa stadi za maisha zinaokoa taifa la kesho vivyo hivyo vizazi vijavyo vya mtoto wa kike vinatakiwa kupewa fursa hiyo.

Kwa mkoa wa Pwani wanafunzi wa kike wameanzisha kazi ya kuuza bidhaa, kutengeneza sabuni ambazo wakiuza wanapata fedha za kununulia baadhi ya mahitaji ambayo yalipaswa kufanywa na wazazi na walezi wao.

Anakumbusha kuwa serikali inapaswa kutenga bajeti kubwa zaidi kwa elimu ya msichana, kujenga shule zaidi, na kutoa masomo kwa wasichana, sambamba na jamii kubadili mtazamo kuhusu umuhimu wa elimu ya msichana na kuunga mkono juhudi za kuhakikisha kwamba wasichana wote wanapata elimu.

Vivyo hivyo, walezi na wazazi wanapaswa kuwahakikishia mabinti kupata elimu na kuwaunga mkono katika masomo yao huku asasi za kiraia zikisaidia kusaidia kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa elimu ya msichana na kutoa huduma za usaidizi kwa wasichana.

Anaeleza kuwa kufundisha stadi za maisha shuleni kunachangia kumwezesha mtoto wa kike kujiamini na kuanza kijitengenezea kipato katika umri mdogo.

Aidha, stadi za maisha ni njia mojawapo ya watoto kuwa na uwezo wa kuwasaidia wengine na kuondokana na hali ya kutegemea wazazi wao muda mwingi huku wakiwa na uwezo wa kumudu kununua baadhi ya mahitaji yao kwa akiba wanazotunza.

Mmoja wa wazazi Cloud Saprapasen, akizungumzia juhudi za Room to Read, anasema stadi za kazi ni ukombozi kwa watoto wa kike.

Saprapasen anasema stadi za maisha kwa watoto wa kike ni muhimu kufundishwa wakiwa wadogo kwani zimekuwa kielelezo cha kuwafanya wajiamini na kuanza kujitegemea wakiwa bado wadogo huku wakiwa vinara wa kuepuka vishawishi.

"Umuhimu wa kuwafundisha watoto stadi za kazi ni kuwawezesha kujiamini na wanawasaidia wengine wakiwamo wazazi na walezi. Pia zinaimarisha usawa kwa kuondoa ubaguzi wakati wa kutoa majukumu kwa watoto," anasema.

Ester Matiku, mwalimu wa Sekondari ya Mwambisi Forest Kibaha anasema stadi za maisha zinazofundishwa zinamtengeneza mtoto wa kike kujitegemea hata akihitimu masomo anajiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa.

"Room to Read inasaidia watoto wa kike kutulia shuleni na kuzingatia masomo, stadi za maisha zinawaandaa kuwa wazalendo, viongozi wa baadaye na wenye kujali utu," anasema.

Anasema wakati wa kufundisha amekuwa akitumia mbinu shirikishi, na njia ya majadiliano ambayo inajenga usawa wa wasichana na wavulana lengo kumfanya mtoto wa kike aweze kuwa jasiri katika kujieleza na kujibu maswali awapo shuleni lakini pia hata akiwa nyumbani.

Ester anasema stadi za kazi zimeleta mabadiliko kwa watoto wa kike moja wapo ni kuachana na utoro, mimba lakini pia watoto wamekuwa wanajiamini kwa kupenda shule na kupigania ndoto zao.

Mwakilishi kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Ramson Chambua, anasema shule za wasichana za bweni katika mikoa 16 zimejengwa na nyingine 10 zitajengwa kuendelea kuhakikisha watoto wa kike wanaosoma katika mazingira salama.

Anasema lengo ni kujenga shule 100 za wasichana za bweni na kwasasa wanaanza kwa kila mkoa ambapo pia aliwakumbusha wazazi na walezi kulinda usalama wa mtoto na kutoa taarifa pale wanapobaini kuna jambo haliendi sawa.

Chambua anasema serikali inaendelea kuzuia mdondoko kwa wanafunzi ambao tayari Shirika la Room to Read limeshafanya huku akisisitiza walimu kufundisha kwa hadithi na mifano ili kuboresha uelewa kwa wanafunzi.

Baadhi ya wanafunzi walionufaika wanasema elimu ya stadi za maisha imewasaidia sasa kutunza fedha wakiwa shuleni na kuanzisha miradi ambayo inawasaidia kununua baadhi ya vifaa pindi wazazi wao wanapokuwa hawana fedha," anaeleza.

Aisha Mussa mwanafunzi wa Nyumbu Sekondari ambaye ni mmoja wa wanufaika wa mradi wa elimu kwa msichana anasema, alianza kuingia katika mradi huo akiwa darasa la tano hadi sasa anaendelea nao umemuimarisha ukilinganisha na alikotoka, akitaja kujiamini.

Anasema awali hakuwa na uwezo wa kuzungumza mbele za watu lakini pia uwezo wake darasani haukuwa wakuridhisha na wanafunzi wengine walikuwa wakimdharau kupitia mradi wa msichana ulimpa ujasiri na kufanya vizuri darasani na hata kwenye uongozi shuleni.

"Nilikuwa kati ya wanafunzi waliodharaulika kwa kuwa na uwezo mdogo shuleni hata nilipoanza kidato cha kwanza nilipangwa darasa ambalo wanafunzi wengi uwezo wao uko chini kupitia mradi wa msichana nilikuwa jasiri wa kusoma kwa bidii na kupata daraja la juu la ufaulu pia niliweza kugombea nafasi za uongozi nikapata na kuwa kiongozi bora jambo ambalo kabla ya mradi sikuwa nalo," anaeleza.



## TOSCI kufungia mbegu zinazouzwa nje ya mfumo

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) Kanda ya Kaskazini imetangaza kuzifungia mbegu ambazo zinauzwa nje ya mfumo wa ruzuku katika maduka yaliyoko mkoa wa Singida hadi hapo zitakapoingizwa katika mfumo huo kama ilivyoelekezwa na serikali.

Mkaguzi kutoka TOSCI, Areth Kibalaza alisema hayo juzi baada ya kufanya ukaguzi kwenye maduka mkoani hapa na kubaini baadhi ya maduka yanaendelea kuuza mbegu za mahindi bila kutumia mfumo wa ruzuku, jambo ambalo ni kosa na linaleta mwanya kuuzwa mbegu ambazo ni feki.

"Tumepita kwenye maduka na mbegu zote ambazo zinauzwa nje ya mfumo wa ruzuku zimefungiwa mpaka pale zitakapoingizwa kwenye mfumo, kwa hiyo mawakala wote wa kuuza mbegu wahakikishe wanazisajiri kwenye mfumo wa ruzuku," alisema.

Mkaguzi Zera Mwankemwa alisema wauzaji ambao walikuwa na mbegu walizokuwa wanauza katika msimu uliopita ambazo hazina stika, wawasiliane kampuni au mawakala waliowaulizia ili zisajiliwe katika mfumo wa ruzuku.

Alisema mbegu zote ambazo hazitasajiliwa kwenye mfumo wa ruzuku hazitaruhusiwa kuuzwa madukani na mfanyabiashara atakayekiuka agizo hilo atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Baadhi ya wakulima walisema utaratibu wa kukagua maduka unaofanywa na TOSCI ni mzuri kwa kuwa unasaidia kudhibiti mbegu feki ambazo zimekuwa zikiingizwa sokoni kinyemela na wafanyabiashara wasio waaminifu.

Walisema serikali kupitia TOSCI iwe inafanya kaguzi kama hizo mara kwa mara kwani kila inafika msimu wa kilimo mbegu zinaanza kuingizwa hali ambayo imekuwa ikisababisha hasara kwa wakulima kwa kupata mazao kidogo.

Wakala wa Pembejeo, Anna Marema, alisema uuzaji wa mbegu kwa kutumia mfumo wa fuzuku umesaidia sana kuongezeka kwa mauzo ya mbegu katika duka lake kwasababu wakulima wanakuwa na uhakika wa kupata mbegu bora katika duka lake.

# Wabunge waibana serikali madeni ya wazabuni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wameibana serikali kuhusu madeni ya wazabuni waliotoa huduma kwenye shule za serikali na makandarasi kwa kuwa yamekuwa ya muda mrefu, hata kusababisha baadhi yao kufilisiwa na benki walizokopa.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Moshi Mjini (CCM), Priscus Tarimo, alihoji mpango wa kuwalipa wazabuni wanaotoa huduma mbalimbali, hususani chakula kwenye shule za serikali ambao wanadai kwa muda mrefu.

Vilevile, akiuliza swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Asia Halamga alisema katika kipindi cha bajeti ya mwaka 2024/25, waziri (hakumtaja) alisema kuwa zimetolewa Sh. bilioni 949 kwa ajili ya ulipaji madeni mbalimbali.

"Ninataka kujua iwapo watoa huduma shuleni kama wapo kwenye fedha hizi na pia ninataka kufahamu wanatakiwa kulipa kwa muda gani ili wananchi hawa wafahamu watakaa muda gani kwa sababu watoa huduma shuleni wengi ni wajasiriamali wadogo wadogo," alisema.

Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA), Grace Tendegu, alisema serikali inasema inafanya uhakiki ndipo ilipe madeni hayo, lakini kuna wazabuni na makandarasi wanadai madeni ya miaka mitatu na kuhoji uhakiki unachukua muda gani ili walipwe fedha zao.

Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA), Cecilia Pareso, alisema miongoni mwa watu wanaodai serikali kwa muda mrefu ni makandarasi wa barabara.

"Watu hawa wanaochukua kazi hizi, wengi wanakwenda kukopa benki wakati wanatakiwa kufanya marejesho. Serikali haijawalipa. Nini kauli ya serikali kwa makandarasi wanaodai na wapo wengine wamefilisiwa kwa sababu walikwenda kukopa?" alihoji.

Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Neema Lugangira, alisema tatizo la madeni ya wazabuni wa chakula shuleni linaathiri upatikanaji chakula na kuathiri pia uwezo wa kusoma kwa watoto.

"Agosti mwaka huu, Naibu Waziri katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Zainabu Katimba alisema bungeni kuwa wamewasilisha Wizara ya Fedha madeni ya wazabuni wa chakula shuleni ya Sh. bilioni 21.7.

"Je, uhakiki huu utakamilika lini na kwa mfano Jimbo la Bukoba Mjini, kuna shule sita za sekondari ambazo ni za serikali ambazo zinadai Sh. milioni 936 na ni kati ya mwaka hadi miaka sita," alisema.

Akitoa majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande alisema serikali inaendelea na utaratibu wa ulipaji madeni mbalimbali, yakiwamo ya wazabuni wa chakula waliotoa huduma katika shule hizo.

Alifafanua kuwa ulipaji huzingatia upatikanaji mapato na uhakiki wa madeni unaofanywa na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali (IAG) na kwamba lengo la serikali kufanya uhakiki ni kutekeleza azma ya usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma kulingana na Sheria ya Bajeti, Sura 439, na Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348.

Alisema Wizara ya Fedha inazielekeza halmashauri zote nchini kulipia huduma mbalimbali wanazopokea kutoka kwa watoa huduma kwa wakati ili kuepuka ulimbikizaji madeni na kuondoa usumbufu usio wa lazima kwa watoa huduma.

Chande alisema watoa huduma shuleni walikuwa sehemu ya wanufaika wa fedha zilizotengwa mwaka jana na kuwa zinaendelea kulipwa hadi mwaka ujao.

"Nimwombe mheshimiwa mbunge na wazabuni wawe na subira, muda ukifika fedha zao zitalipwa, uhakiki utakapokamilika na mapato yakipatikana watalipwa wazabuni wote pamoja na makandarasi," alisema.



Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa (kushoto), akimsikiliza Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, nje ya Ukumbi wa Bunge mjini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bila mazingira bora ya kazi kwa walimu, elimu bora itakuwa ndoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Shirika la Action Aid Tanzania, Bavon Christopher, amesema licha ya serikali kujenga miundombinu mingi ya madarasa, kama mazingira ya ufanyaji kazi kwa walimu hayataboreshwa, elimu bora nchini haitapatikana.

Christopher, alibainisha hayo juzi jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye kikao na wadau kutoa matokeo ya utafiti uliofanywa na shirika hilo kuhusu kazi zenye staha kwa walimu wanawake katika maeneo ya vijijini.

"Tupo hapa kwa ajili ya kusambaza matokeo ya utafiti wa kazi zenye staha kwa walimu wanawake hasa katika maeneo ya vijijini kwasababu Action Aid inafanya programu za elimu na tunahakikisha kwamba katika kuboresha ubora wa elimu tunangalia pande mbili pande ya mazingira ya wanafunzi lakini pia upande wa walimu.

"Sasa kwa uzoefu wetu tumekuwa tukiona mara nyingi walimu wamekuwa na mazingira mabovu ambayo hayafai hali halisi ya miundombinu yao ya kufundishia, madarasa kupatikana kwa vitabu nyenzo mbalimbali, lakini vile vile ofisi zao unaingia kwenye ofisi ya walimu unakuta ni kama stoo," alisema.

Alisema shule nyingi zinawalimu wengi ambao hawana nyumba za kuishi hasa vijijini hali ambayo inawalazimu wengi wao kutembea umbali mrefu kwenda kwenye vituo vyao vya kazi.

"Tumeona kwamba hata tukifanya vipi hata tukijenga majengo mazuri ya madarasa lakini kama mazingira ya walimu hayawezi kuboreshwa elimu haiwezi kuwa bora hata mara moja kwahiyo tumefanya utafiti huu kuweza kuangalia hadhi ya kazi yenye staha za walimu wa kike hasa sehemu za vijijini na utafiti wetu umeonyesha mambo mbalimbali," alisema.

Alisema mambo hayo ni pamoja na mazingira ya taaluma jinsi gani mwalimu anatakiwa aendelezwe kitaaluma imekuwa ni changamoto ambayo inawafanya walimu wasiwe na uwezo mzuri wa kufundisha au kutoa maarifa kwa wanafunzi.

"Lakini tumeangalia mazingira halisi nyumba vijijini zimekuwa ni hafifu na zisizokuwa na uwezo sehemu nyingine unakuta nyumba haina hata umeme, ofisi hamna wakati mwingine walimu wanatumia madarasa kama ofisi wakati mwingine walimu wanarundikana kwenye ofisi ndogo ukiingia unakuta vitabu, karatasi za wanafunzi chaki kila kitu ndani ya ofisi ndogo yaani ni kama stoo," alisema.

Alisema utafiti huo pia umeangalia malipo ambapo mishahara ni midogo hali ambayo inasababisha baadhi ya walimu kutofundisha vizuri na kujihusisha na mambo mengine ya kujitafutia riziki.

"Kwa sababu kama mwalimu anafamilia na mshahara hautoshi mwisho wa siku atangalia mazingira mengine ya kujaribu kujipatia kipato sasa hiyo inashusha uwezo wa mwalimu kufundisha," alisisitiza.

Kadhalika, alisema katika utafiti huo wameangalia haki ya masaa ya kazi walimu wakiwa wachache mwalimu mmoja itabidi achukue majukumu makubwa.

Alisema kwa mujibu wa sera ya elimu mwalimu mmoja anatakiwa afunishe wanafunzi wasio zaidi 40, lakini wakati mwingine darasa moja wanafunzi zaidi ya 80.

Ofisa Elimu Awali na Msingi Wilaya ya Mafia, Ephata Kaale, alisema utafiti huo umekuja wakati mwafaka kwa kuwa bado walimu wengi nchini hasa katika maeneo ya vijijini wanakabiliwa na changamoto mbalimbali.





# Waliokosa mawasiliano miaka 40 sasa kuyapata

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI wa Kata ya Ikondo, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wanatarajia kuondokana na adha ya mawasiliano ya simu kwa zaidi ya miaka 40 baada ya serikali kuanza ujenzi wa mnara.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Mbunge wa Lupembe, Edwin Swalle alipozungumza na waumini wa Kanisa Katoliki Parokia ya Matembwe, wilayani Njombe.

Swalle alisema kutokana na tatizo la mawasiliano linalowakabili wananchi hao kwa miaka mingi ambapo hali hiyo inasababisha kuzorotesha uchumi wao.

"Hatimaye kilio cha wananchi kimesikika serikali tayari imeshapeleka makandarasi katika kata hiyo ya Ikondo tayari kwa kuanza ujenzi wa mnara huo mara moja," alisema Swalle.

Swalle alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusikiliza na kutatua kero za wananchi na kufanya matatizo yanayowakabili kuwa historia.

"Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo uboreshaji wa huduma kama katika sekta za afya, elimu, barabara ambazo zimefunguliwa kutoka kata moja kwenda nyingine, kijiji kwa kijiji na hii yote ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora," alisema Swalle.

Awali Paroko wa Parokia ya Matembwe, Edward Msigwa aliwataka wananchi kushiriki shughuli za maendeleo katika maeneo yao na kwamba kwa kufanya hivyo kuna leta tija kwa jamii na serikali.

Baadhi ya wananchi wa kata ya Ikondo wamesema kujengwa mnara wa mawasiliano katika kata hiyo kunakwenda kufufua uchumi wao kwa kuwa walikuwa wanashindwa kuwasiliana na wafanyabiashara kununua mazao.

Mmoja wa wananchi hao, Israel Mhada alisema kujengwa mnara wa simu katika kata yao kutasaidia kukuza uchumi wao kwa sababu watakuwa na mawasiliano ya uhakika.

"Tunamshukuru sana mbunge wetu na serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa sababu tutapata mawasiliano katika uongozi wake, huko nyuma tulipata shida kupata mawasiliano kama vile tupo dunia ya peke yetu," alisema Mhada.

Aldo Msimike alisema kutokana na umuhimu wa teknolojia hivi sasa kata yao ilikuwa nyuma kwa sababu ya kushindwa kufanya biashara zao kisasa badala yake walikuwa wanakikisia ili kufika mjini Njombe na kuuza bila ya makubaliano.

## Urasimishaji ardhi waondoa migogoro ya mipaka Makambako

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

WANANCHI wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, wilayani Njombe wamesema zoezi la urasimishaji ardhi linaloendelea katika maeneo yao limesaidia kuondoa migororo ya mipaka ambayo imekuwa inawakabili na kusababisha ugomvi miongoni mwao.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na wananchi wa mitaa ya Kilimahewa na Mashujaa iliyoko Halmashauri ya Mji wa Makambako wakati wakizungumza na Nipashe.

Walisema zoezi hilo limesaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikijitokeza hasa pale wanawake wanapofiwa na waume zao.

Wananchi hao, akiwamo Yusto Chungu, walisema licha ya utaratibu huo kuondoa migogoro ya kimpaka, pia litasaidia kupanga mji pamoja na kukuza uchumi wao kwa kuwa kupitia hatimiliki watakazopewa, zitawawezesha kunufaika na mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha.

Dorice Lunyungu alisema zoezi hilo limekuja wakati sahihi kwa sababu huko nyuma watu walikuwa wananyang'anywa hadi kutapeliwa kwa sababu ardhi inakuwa haijarasimishwa.

Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Kilimahewa, Izack Lupenza, alisema zoezi hilo limeondoa changamoto ya migogoro ya ardhi iliyokuwa imekita mizizi katika eneo lake la uongozi.

"Kwa kweli kipindi cha nyuma hali ilikuwa ni mbaya kwa sababu ilikuwa haiwezi kupita siku nzima hujapokea kesi ya mgogoro wa ardhi na ilikuwa inasumbua muda mrefu, inabidi utafute watu wa zamani wanaojua historia ya eneo husika," alisema Lupenza.

Ofisa Maendeleo ya Ardhi katika Halmashauri ya Mji wa Makambako, Flaviana Mamkwe alisema zoezi hilo linaendelea kwenye mitaa 19, huku akiwataka wananchi ambao mitaa yao inarasimishwa ardhi kutumia fursa hiyo ili kuondokana na migogoro isiyo na sababu.

Mamkwe alisema zoezi hilo linatakiwa kukamilka ndani ya miezi sita, hivyo wananchi wanapaswa kujitokeza kuhakiki taarifa zao sambamba na kukamilisha michago ili kuweza kupima mtaa mzima ili mwananchi aweze kupatiwa hati miliki.




Mkurugenzi wa Kampuni ya JATU PLC, Peter Gasaya, akitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana katika kesi inayomkabili yenye makosa mawili, likiwamo la kujipatia Sh. bilioni 5.1 kwa njia ya udanganyifu. Kesi hiyo imeahirishwa kutokana na upelelezi kutokamilika. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## DC awapongeza wananchi wanaojitolea ujenzi miradi

**Na Mwandishi Wetu,** ILEJE

MKUU wa Wilaya ya Ileje, mkoani Mbeya, Farida Mgomi, amewapongeza wananchi wa kijiji cha Chabu, Kata ya Bupigu kwa kujitolea katika ujenzi wa zahanati ya kijiji.

Alisema wananchi hao wamechangia malori 10 ya mchanga na kuchimba mashimo manne yenye thamani ya Sh. milioni 1.5, mradi ukigharibu Sh. milioni 69.4.

Mgomi aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea na kukagua maendeleo ya mradi huo na kupongeza juhudi hizo ambazo alisisitiza zinapaswa kuungwa mkono na wananchi wa maeneo mengine.

"Wananchi mmeonesha mfano wa kuigwa kusimamia mradi wenu kikamilifu, lakini pia kujitoa kushiriki kutekeleza mradi kwa zaidi ya Sh. milioni 1.5.

"Fedha iliyotolewa na serikali inaweza isitoshe kutekeleza mradi kama ambavyo wananchi mnataka, lakini kama ikitosha na inayobaki ina maana inaendeleza kazi nyingine za mradi kulingana na mahitaji ya wananchi," alisema.

Alisema utekelezaji wa mradi huo unalenga kujenga matundu sita ya vyoo. Kati yake, mawili ya wagonjwa, mawili ya wahudumu, bafu na choo cha wajawazito na kingine cha wenye mahitaji maalumu.

Mgomi alisema mradi huo pia unahusisha kichomea taka, shimo la majivu, shimo la kondo la mama wajawazito, kitakasa mikono na uwekaji mfumo wa maji.

Awali Mganga Mfawidhi wa Zahanati hiyo, Dk. Diannaeose Massawe, alisema mradi huo umeshatumia Sh. milioni 50.7 sawa na asilimia 73.2 na fedha zilizosalia Sh. milioni 18.7 zitatumika katika shughuli zilizosalia.

Alisema mradi umefikia asilimia 93 ya utekelezaji wake, hivyo uko katika hatua nzuri za utekelezaji.

**"Fedha iliyotolewa na serikali inaweza isitoshe kutekeleza mradi kama ambavyo wananchi mnataka, lakini kama ikitosha na inayobaki ina maana inaendeleza kazi nyingine za mradi kulingana na mahitaji ya wananchi," alisema.**



## Umeme pasua kichwa Zenji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania kukabiliana na tatizo la umeme visiwani hapa.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini, John Joseph Kilangi, alitangaza mpango huo katika kikao cha watendaji wa wizara hizo kilichofanyika visiwani hapa jana.

Kilangi, alisema hatua hiyo imekuja baada ya kubaini kuwa Zanzibar imekuwa ikipata umeme mdogo kwenye njia zake hasa kutoka gridi ya Taifa Tanzania Bara.

Alisema kituo cha umeme Mtoni kitakiwa kupokea kilovoti 132, lakini kiwango kinachofika ni 110 na kusababisha baadhi ya vitendea kazi, ikiwamo tranfoma kushindwa kufanya kazi.

Alisema hali hiyo imekuwa ikitokea kituo cha umeme cha Dar es Salam kinapokuwa kinafanyiwa matengenezo.

Kilangi, alisema nishati ni sekta muhimu kwa uchumi na ni injini ya maendeleo ya nchi yoyote duniani.

Alisisitiza kuwa uwekezaji hauwezi kuendelea kama nishati hiyo inakabiliwa na changamoto na Zanzibar kwa kiasi kikubwa inategemea utalii kukuza maendeleo, hivyo bila umeme mambo hayawezi kwenda vizuri.

Hata hivyo, alisema kuna mkakati wa joto la ardhi kutumika kuzalisha umeme kwa wingi iliyogundulika kusini mwa Tanzania Bara katika Mkoa wa Mtwara.

Alisema kuna uwezekano wa kuzalisha karibu megawati 5,000 katika chanzo hicho na mpango huo utakapoanza Zanzibar itanufaika.

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhandisi Felchesmi Mramba, alisema wanafahamu kuwa Zanzibar imekuwa ikipata umeme mdogo kutokana na kifaa kinachotoa kutoka bara kuanza kuzidiwa na matumizi kuongezeka.

Mramba, alisema kikao hicho kitajadili jinsi ya kukabiliana na tatizo hilo kwa kuongezea vifaa zaidi vya kutoa umeme kutoka Dar es Saalam kuja Unguja na kingine Tanga hadi Pemba.

Alisema hatua zimeanza kufanyika ikiwamo upembuzi yakinifu chini ya Bahari ya Hindi, kukamilisha mazungumzo ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) kwa ajili ya kupata fedha za mkopo na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuanza mpango wa kumpata mshauri wa kusimamia mradi huo.

# ACT yazungumzia chama kikongwe kubwagwa uchaguzi Botswana

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema chama cha upinzani cha Umbrella For Democratic Change (UDC) cha Botswana kushinda uchaguzi ni kuvuma kwa pepo za mabadiliko ya demokrasia katika nchi za kusini mwa Afrika.

Kimesema kushindwa kwa Chama cha BDP kilichotawala kwa miaka 58 nchini humo ni nguvu mpya ya kizazi cha sasa kuvikataa vyama vikongwe.

Naibu Katibu Mkuu wa ACT Wazalendo Zanzibar, Omar Ali Shehe, aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe kufuatia ushindi wa UDC nchini humo katika uchaguzi uliofanyika hivi karibuni kwa kuvishirikisha vyama vingi vya siasa.

Shehe, alisema matokeo yaliotangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Botswana na kukipa ushindi UDC ni kengele ya mageuzi ya kisiasa iliyopigwa kitambo na kuviondoa vyama vikongwe kuanzia Malawi, Zambia, Kenya, Botswana huku ANC cha Afrika Kusini kikiponea chupuchupu kushindwa.

Alisema upepo huo ni wazi kwa sasa unaelekea kuvipeperusha vyama vyote vikongwe katika nchi hizo za Kusini mwa Afrika kutokana na utashi wa kizazi hicho kuheshimu zaidi nguvu ya demokrasia na mabadiliko ya umma kufikia mageuzi ya kweli.

"Huu ni wakati mpya wa kizazi cha mabadiliko. Zanzibar mwakani kutapita kimbunga tsumani cha demokrasia na kukisomba Chama Cha Mapinduzi. Iwe isiwe, CCM hakiwezi kuhimili kishindo cha maadiliko," alijigamba Shehe.

Aliongeza kusema kuwa wimbi la mabadiliko hayo lilianza mataifa ya kaskazini, yakaelekea magharibi mwa Afrika na sasa kusomba vyama vya kusini mwa Afrika baada ya Afrika Mashariki huko Kenya na kuwa mfano wa mabadiliko.

Naibu katibu mkuu huyo, alisema ACT kimejiandaa kushiriki uchaguzi huo ambao anaamini CCM kitaondoka madarakani kwa njia za kiungwana kama BDP kilivyoachia utawala Botswana.




Kifaa cha kutunzia chupa za plastiki zilizotumika kikiwa kimewekwa katika kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, Dar es Salaam jana. Kwa mujibu wa abiria kimewekwa na uongozi wa Wilaya ya Ubungo ili kuzuia utupaji ovyo wa chupa hizo kituoni hapo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wizara kuzidi kutangaza utalii Z'bar kimataifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale zitaendelea kuitangaza Zanzibar kimataifa kwa kuweka mazingira bora ya utalii.

Abdula alitoa kauli hiyo kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi wakati wa kukabidhi zawadi kwa washindi wa mbio za kimataifa za marathon yaliyofanyika viwanja vya Forodhani visiwani hapa.

Alisema kwa kipindi kirefu Zanzibar imejikita katika utalii wa msimu na kuvutia wageni wengi kutembelea maeneo ya kihistoria ya mji mkongwe na ya bahari.

Alisema jumla ya watalii 600,300 wametembelea Zanzibar kwa mwaka huu.

Abdula, Zanzibar imejaliwa kuwa na eneo kubwa la bahari na kutumika vizuri kwenye utalii kwamba inaweza kuongoza ukanda wa Afrika katika utalii wa michezo ya baharini.

Aliwataka wadau kujitokeza kuendeleza michezo ikiwamo ya mbio za marathon, pikipiki baharini, kuogelea na ngalawa ili kuvitangaza visiwa hivyo vya Unguja na Pemba kimataifa.

Kwa mujibu wa Abdula, serikali imepanga kujenga uwanja mpya wa mpira wa miguu na kutumika katika mashindano ya fainali ya Mataifa ya Afrika (AFCON) mwaka 2027 na kuvifanyia ukarabati mkubwa viwanja vya New Amani Complex na Gombani Pemba kulingana na viwango vya kimataifa.

Aliwataka wanamichezo na wananchi kuendelea kulipa kodi na kudai stakabadhi wanaponunua bidhaa na kwa wafanyabiashara kutoa wanapofanya mauzo ili kuziba mianya ya upotevu wa mapato ya serikali na kupiga hatua katika maendeleo.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, alizipongeza kampuni za Tigo na Zantel kwa kuendelea kutumia eneo la Ngome Kongwe kama kituo cha kuanzia mashindano ya mbio hizo na kuzidi kutangaza urithi huo wa mji Mkongwe na utalii.

Alisema mashindano hayo yanatoa fursa kwa mataifa na washiriki kupata nafasi ya kutembelea vivutio vya utalii vilivyoko visiwani hapa na kuitangaza Zanzibar wakati wanaporejea nchini mwao.

Mwenyekiti wa mashindano hayo, Hassan Mussa alisema wanapongeza hatua za Rais Mwinyi kuboresha miundombinu ya michezo kwa kujengwa viwanja vipya na vya kisasa vya michezo na barabara ambazo ni rafiki kwa wanariadha.

Alisema Tigo/Zantel kwa kushirikiana na wadau wengine wa Zanzibar mashindano ya mbio hizo za Marathon wataendelea kuunga mkono juhudi za Rais Mwinyi za kuimarisha sekta ya michezo nchini kwa kipindi chake cha uongozi cha miaka 10.

Ofisa Mkuu wa Biashara wa Tigo/ Zantel, Isack Nchunda, alisema wataendelea kudhamini mashindano hayo na mengine ili kuiunga mkono serikali na kuendeleza vipaji vilivyoko nchini kupitia michezo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ASHURA MUHSIN ABUBAKARI** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne, chenye index namba P 2633/0003/2015 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SAMBU SECONDARY SCHOOL CENTRE. Mwaka 2022.** Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi . Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN//238498/2024**

## TANGAZO LA KAZI/UALIMU

Tunatangaza nafasi za kazi ya ualimu mchepuo wa kingereza kwa masomo yote na madarasa yote kuanzia chekechea Hadi darasa la saba, sifa za chekechea ni certicate au diploma na kwa darasa la kwanza Hadi la saba ni diploma au shahada ya kwanza ya elimu.

**Mawasiliano 0783298900**

## KUPOTEA KWA BARUA YA OFA YA KIWANJA

**THECLA WANKURU KOHI** anatangaza katika nafasi kama msimamizi wa mirathi, kupotea kwa Barua ua ofa (Letter of offer) ya **kiwanja no 415.** Kilichopo chini ya jina la Yadon Mtarima Kohi, kilichopo Jangwani Beach, Dar es Salaam. Yoyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi **PHQ/DAR/KIN/240321/2024**

## KUPOTEA KWA BARUA YA OFA YA KIWANJA

**THECLA WANKURU KOHI** anatangaza katika nafasi kama msimamizi wa mirathi, kupotea kwa Barua ya Ofa (Letter of Offer ) ya kiwanja **no. 77** Kitalu D kilichopo chini ya jina la Yadon Mtarima Kohi, kilichopo Tegeta, Dar es Salaam. Yoyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi : **PHQ/DAR/KIN/240353/2024.**

## TANGANZO, TANGAZO MNADA WA NYUMBA

FAGIO BROKERS KWA IDHINI TULIYOPEWA NA HATOSWI/SAJFA MICROFINANCE CO. LTD, TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA NYUMBA MOJA MALI YA RAYMOND A. MWAMPALANJE ILIYOPO KITONGOJI CHA SWILA, KIJIJI CHA NZUNDA – RUNGWE.

MNADA UTAFANYIKA SIKU YA JUMAATANO TAREHE 30/10/2024 KUANZIA SAA 5:00 KAMILI ASUBUHI ENEO NYUMBA ILIPO.

MASHARTI YA MNADA

1. MNUNUZI ATATAKIWA KULIPO 25% YA BEI YA NYUMBA NA SALIO LA 75%LIMALIZIWE NDANI YA SIKU KUMI NA NNE KUANZIA TAREHE YA MNADA.
2. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI

**MAWASILIANO 0768224862/0758063383**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**CIVIL CASE NO.26907 OF 2024**

**MOHAMMED INTERPRISES (TANZANIA) LIMITED—-PLAINTIF**

**VERSUS**

**BOAZ ANYITIKE KYANDO——————- DEFENDANT**

**TO: BOAZ ANYITIKE KYANDO**

**TAKE NOTECE** that hearing of the above suit has been set down for Mention on 07 day of 11, 2024 at 08:30am in foreman thereafter at district court You must produce on that day all the witnesses upon whose evidence and all the document upon which you inted really in support of your case

Given under my hand and the seal of this 25th day of 10,2024.

DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE I/C
KYELA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBLA WILAYA YA DODOMA MAHALI DODOMA**

**MAOMBI MADOGO NA.189 YA MWAKA 2024**

**BAINA YA**
**ALFA M SONYO........................................................................ MDAI NA WENZAKE.**

**DHIDI YA**

**1. KEDMOND M CHILONGOLA.......................................MDAIWA**

**KWA:**
**KEDMOND M CHILONGOLA**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yoyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 06.11.2024 saa 3.00 asubuhi Kwa ajili ya kutaja.
ANGALIZO: -Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 09 ya Mwezi wa OCTOBER, 2024.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**

**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa GEITA**

**Shauri a madai/Ndoa Na 77/2024**

**Jina la Mdai: PENDO GERLD MASOLWA**

**Jina la Mdaiwa: PETER LEONARD**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuniya 18 ya kanuni za taratibu Madai katikamahakamazaMwanzo)**

**Kwa:PETER LEONARD**
**WA GEITA**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba **:MADAI YA TALAKA** Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 6 Mwezi 11 Mwaka 2024 saa 08.30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:**Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo **Tarehe 28 Mwezi 10 Mwaka 20**24

HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE
GEITA.

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 75 LA 2024**

**SAADA ABDALAH LAIZA MUOMBAJI /WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**(1) J.J RECOVE**
**(2) AGNES MWAKIPESILE RAZALO MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**(1) J.J RECOVE**
**(2) AGNES MWAKIPESILE RAZALO**
**POPOTE ULIPO/MLIPO:**

**SAADA ABDALAH LAIZA.** Amefungua /wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 19/11/2024 saa 03.00 Asubuhi/Mchana mbele ya **Mh J.W.SILLAS.** Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutia Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 24 Mwezi 10 Mwaka 2024

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAOMBI YA GHARAMA NA. 19995 YA MWAKA 2024**
**TATA AFRICA HOLDING TANZANIA LIMITED ........................MUOMBAJI**
*DHIDI YA*
**GREEN DIAMOND JOINT STOCK COMPANY .............................MDAIWA**

**KWA:**
GREEN DIAMOND
JOINT STOCK COMPANY
**DAR ES SALAAM.**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mwombaji aliyetajwa hapo juu amefungua shauri dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati ya Madai zinazopatikana katika Mahakama hii, unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii, wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe **5/11/2024** saa tatu 11:00) asubuhi mbele ya Mhe. **A.H. MBADJO** Kwa ajili ya kusikilizwa.

**ANGALIA:**
Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikathibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.

**HATI** hii imetolewa kwa **MKONO** wangu na **CHAPA** ya Mahakama leo hii tarehe 24 Mwezi NOV 2024.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,

KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Watu 14 wauawa kwa radi Uganda

**KAMPALA,** Uganda

JESHI la Polisi nchini Uganda limesema mlipuko wa radi uliopiga kwenye kanisa moja nchini humo umeua takriban watu 14 na kuwajeruhi 34 walipokuwa wamekusanyika kwa ajili ya maombi.

Taarifa ya polisi ilisema tukio hilo lilitokea jana katika kanisa lililokuwa ndani ya kambi ya wakimbizi ya Palabek wilayani Lamwo Kaskazini mwa Uganda.

"Waathiriwa...walikuwa wamekusanyika kwa ajili ya maombi wakati mvua ilianza kunyesha mwendo wa saa 11:00 jioni na radi ilipiga saa kumi na moja unusu," polisi walisema.

Aidha, ilielezwa kuwa polisi hawakutambua uraia wa waathiriwa lakini kambi hiyo na zingine katika eneo hilo zinahifadhi wakimbizi kutoka Sudan Kusini.

Pia ilielezwa kuwa wengi wa wakimbizi hao walikuwa wamekimbia wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyosababisha umwagaji damu vilivyoikumba nchi hiyo muda mfupi baada ya uhuru wake mwaka 2011.

Hata hivyo, taarifa hiyo ya polisi ilisema waasiri wa wengi walikuwa vijana pamoja na msichana wa miaka tisa.

Vile vile, ilitajwa kuwa dhoruba mbaya za radi ni za kawaida katika nchi hiyo ya Afrika masharik, haswa katika majengo ya shule ambako mara nyingi yanakosa vikondakta vya kudhibiti radi. **TRT**

## 13 wauawa na RSF Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

TAKRIBANI watu 13 wameuawa kwa kupigwa risasi katika shambulizi linalodaiwa kufanywa na kundi la wanamgambo la (RSF) katika jimbo la Al-Jazira kusini mwa Khartoum nchini Sudan.

Chanzo kimoja kilichozungumza kwa sharti la kutotambulishwa, kililiambia shirika la habari la Ufaransa AFP, kana kwamba kikosi cha RSF, kiliwafyatulia risasi watu hao waliokuwa katika mji wa Al-Hilaliya.

Ilielezwa kuwa jimbo la Al-Jazira nchini Sudan limekuwa eneo kuu la mapigano kutokana na kutoka kwenye kikosi hicho cha RSF kwa kamanda mmoja Abu Aqla Kaykal.

Katika hatua nyingine, ilielezwa kuwa siku chache zilizopita Kaykal alijiunga na jeshi la Sudan, pamoja na kile ambacho jeshi hilo lilieleza kuwa idadi kubwa ya wapiganaji wake, katika tukio la kwanza la kujiondoa kwa ofisa wa ngazi ya juu kutoka kikosi hicho cha RSF.

Hata hivyo, kwa mujibu wa mratibu wa misaada ya kibinadamu wa Umoja wa Mataifa (UN) nchini Sudan, Clementine Nkweta Salami (pichani), RSF ilianzisha mashambulizi makubwa katika maeneo ya mashariki ya jimbo la Al-Jazira kati ya Oktoba 20 na 25, mwaka huu.

Nkweta-Salami ameongeza kuwa wanamgambo hao walitekeleza mauaji ya watu zaidi ya 120 katika mji wa Sariha nchini humo, na kwamba unyanyasaji wa kingono, uporaji mkubwa wa masoko na nyumba pamoja na uteketezaji mkubwa wa mashamba ni miongoni mwa matukio yaliyotekelezwa katika eneo hilo.



Vile vile, ilielezwa kuwa mzozo nchini Sudan ulizuka katikati ya mwezi wa Aprili 2023 kati ya jeshi la serikali linaloongozwa na Abdel Fattah al-Burhan, na kundi la RSF linaloongozwa na naibu wake wa zamani Mohamed Hamdan Daglo. **DW**





Wagombea urais wa Marekani Makamu Rais Kamala Harris na rais wa zamani, Donald Trump, wakizungumza katika mikutano yao ya kampeni. **PICHA: AFP**

## M23 yaendelea kudhibiti maeneo DRC

**KINSHASA,** DRC

WAASI wa M23 wamechukua udhibiti wa mji wa Kamandi Gite, katika eneo la Lubero huko Kivu Kaskazini, ambao uko zaidi ya kilomita 130 kaskazini mwa mji wa Goma.

Ilielezwa kuwa M23 waliuteka mji huo jana baada ya kufanya mashambulizi dhidi ya ngome za Wazalendo, wanamgambo wanaoshirikiana na Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Pia ilielezwa kuwa mapigano yameripotiwa katika eneo la Masisi, katika kijiji cha Kahira. Huku wakazi wakieleza kutokea kwa milipiko mikali na silaha nzito, na kwamba kaskazini mwa eneo hilo milio ya risasi pia ilisikika jana jioni katika Bandari ya Kamandi.

Kwa mujibu wa duru za kuaminika, waasi hao walifanya shambulio la kushtukiza juzi Jumapili asubuhi likilenga ngome za Wazalendo.

Vyanzo vya ndani na hospitali, vilibainisha kuwa baada ya milipuko na milio ya silaha nzito, wapiganaji wa M23 walifanikiwa kuuteka mji huo bila upinzani mkubwa.

Mwanachama wa mashirika ya kiraia kutoka Kamandi Gîte alieleza kuwa mamia ya wapiganaji hao, walikuwa wamejihami kwa silaha za kutosha, na kwamba wananuia kuelekea Butembo.

Ilielezwa kuwa Kamandi Gîte ambayo inapatikana kwenye ufuo wa Ziwa Edward, inayofungua njia kuelekea eneo la Beni, mashambulizi hayo yaliyofanywa na waasi kwa sasa yamesababisha watu wengine kuyahama makazi yao.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa mapigano hayo yanafanyika huku mchakato wa Luanda ukiwa umepiga hatua.

Vile vile, ilielezwa kuwa wataalamu kutoka DRC na Rwanda wamekubaliana juu ya mpango wa kutenganisha majeshi na kuwaondoa waasi wa Kihutu wa FDLR.

Ilielezwa kuwa makubaliano hayo yataidhinishwa na mawaziri wakati wa duru inayofuata ya mazungumzo Novemba 16, mwaka huu huko Luanda. **RFI**

## Marekani kufanya uchaguzi urais leo

**WASHINGTON,** Marekani

WANANCHI nchini Marekani wanafanya uchaguzi wa urais leo baada ya kampeni za wagombea kuhitimishwa juzi Jumapili huku wafuatiliaji wa masuala ya siasa duniani kote wakielekeza macho na masikio yao katika kinyang'anyiro hicho kinachotazamiwa kuwa na upinzani mkali.

Ilielezwa kuwa mgombea urais wa Chama cha Democratic Kamala Harris alihitimisha kampeni zake huko Michigan, huku mpinzani wake wa Chama cha Republican Donald Trump akisimama katika majimbo matatu ya mashariki yenye ushindani mkali.

Ilielezwa kuwa kura za maoni zilionyesha ushindani mkali wa karibu sana kihistoria na ukusanyaji maoni uliofanywa na New York Times na Siena uliochapishwa juzi, ambao umewaonyesha Makamu wa Rais Harris na Rais wa zamani Trump wakiwa sawa katika majimbo saba ambayo huenda yakaamua matokeo ya leo.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa kura nyingine ya maoni ilionyesha Harris akiongoza katika jimbo la Iowa ambalo Trump alishinda kwa urahisi katika chaguzi mbili zilizopita, na hivyo kuongeza uwezekano wa matokeo yasiyotarajiwa, ingawa kura nyingine ilionyesha akiwa nyuma katika jimbo hilo.

# SIMBA QUEENS, YANGA PRINCESS MZIGONI LEO

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kusimama kwa takriban wiki tatu, Ligi ya Soka Wanawake Tanzania Bara msimu wa 2024/25, itaendelea tena leo kwa michezo yote mitano itakayopigwa kwenye viwanja mbalimbali nchini.

Mara ya mwisho ligi hiyo ilichezwa Oktoba 14, huku leo ikitarajiwa kuingia kwenye raundi ya tatu, wakati Mabingwa Watetezi, Simba Queens watakapokuwa ugenini, Uwanja wa Samora, Iringa kucheza dhidi ya Ceasiaa Queens, huku Yanga Princess ikishuka Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam kupepetana na Mashujaa Queens.

Washindi wa Ngao ya Jamii msimu huu, JKT Queens, watakuwa nyumbani, Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo wakiikaribisha Mlandizi Queens, wakati, Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Fountain Gate Princess itaialika Alliance Girls.

**Mchezo mwingine wa raundi ya tatu wa Ligi Kuu, utachezwa Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati, Manyara pale, Get Programs itakapokipiga dhidi ya Bunda Queens.**

Mpaka sasa tayari kila timu imeshacheza raundi mbili, huku Simba Queens ikiongoza kwa kuwa na pointi sita, ikishinda michezo yote, mabao sita ya kufunga na kuruhusu bao moja, ikifuatiwa na Mashujaa Queens yenye pointi nne kwa kucheza mechi mbili, ikishinda moja na sare moja.

JKT Queens inashika nafasi ya tatu na pointi zake nne, lakini imeruhusu mabao mawili nyavuni, huku Mashujaa wakiwa hawajaruhusu bao.

Ceasiaa Queens ipo nafasi ya nne ikiwa na pointi tatu, Bunda Queens nafasi ya tano baada ya kujikusanyia pointi mbili, Yanga Princess ikishika nafasi ya sita pia ikiwa na pointi mbili.

## *Shime alia na umakini mdogo Stars*

Na Faustine Feliciane

BAADA ya juzi kikosi cha Taifa Stars kufungwa kwa mikwaju ya penalti 6-5 na Sudan kwenye mechi ya kuwania kufuzu kwa fainali za Wachezaji Wanaocheza Ligi za Ndani (CHAN), Kocha wa timu hiyo, Bakari Shime, amesema wachezaji wake walikosa umakini kwenye mchezo huo wa marudiano.

Stars licha ya kupata ushindi wa bao 1-0 ndani ya dakika 90, ilipoteza katika changamoto ya mikwaju ya penalti kwenye mchezo huo wa marudiano na kufanya matokeo ya jumla kuwa 1-1 kutokana na Sudan nayo mchezo wa nyumbani kupata ushindi kama huo.

Bao hilo pekee la jana Stars liliwekwa kimyani na Crispian Ngushi dakika ya 32 na kudumu kwa muda wote wa mchezo.

Penalti za Sudan zilifungwa na Walieldin Khidir, Mohamed Abdulrahman, Salaheldin Adil, Ramadan Agab na Ally Abdallah, huku za Stars zikizamishwa nyavuni na Shekhan Ibrahim, Daud Brayson, Abdallah Said, Sabri Kondo na Abdulkarim Kassim, huku Paul Peter mkwaju wake ukipanguliwa na golikipa Ahmed El Fatih.

Hata hvyo, licha ya kupoteza mchezo huo, Taifa Stars imefuzu kushiriki fainali hizo zitakazofanyika mwakani hapa nchini, Kenya na Uganda kwa sifa ya kuwa mwenyeji.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Shime alisema wachezaji wake walicheza vizuri ingawa walipoteza umakini kidogo kwenye kutumia nafasi walizozitengeneza.

"Vijana walipambana, wamecheza vizuri, lakini nadhani yapo makosa madogo ambayo yametugharimu na kufikia hatua ya kupigiana penalti, tulitengeneza nafasi, lakini hatukuzitumia," alisema Shime.

Alisema watafanyia kazi maeneo ambayo wameona yanahitaji nguvu ili kuwa na kikosi imara zaidi na kufanya viziru kwenye mashindano hayo.

Mashindano hayo ya Afrika kwa wachezaji wa ndani yatafanyika mwakani kwa mara ya kwanza hapa nchini, Kenya na Uganda, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya uwenyeji wa fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027.

**SARAKASI...**




Wanafunzi wa Shule ya Msingi Hazina ya Magomeni, wakionesha umahiri wao wa michezo mbalimbali ikiwamo sarakasi wakati wa mahafali ya Shule ya Awali na Msingi mwishoni mwa wiki, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## JKU yapoteana mbio za ubingwa Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HALI ya Bingwa Mtetezi wa Ligi Kuu Zanzibar JKU SC, katika mbio za kutetea taji lake hilo, imezidi kuwa mbaya baada ya kuambulia sare tena katika mwendelezo wa ligi hiyo inayoshirikisha jumla ya timu 16 kutoka Unguja na Pemba.

Maafande hao wa JKU wamejikuta wakilazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Junguni FC, mchezo uliochezwa mwishoni mwa wiki katika Uwanja wa New Amaan Compelex, Unguja.

Matokeo hayo yanaifanya JKU mpaka sasa kuangukia nafasi ya nane katika msimamo wa ligi hiyo kwa kufikisha alama 13 katika michezo tisa iliyocheza.

Maafande hao katika michezo hiyo wameshinda mitatu, sare nne na kufungwa mechi mbili.

Kwa matokeo hayo ambayo mabingwa hao watetezi wanaendelea kuyapata, yanawafanya mashabiki wa soka visiwani hapa kuanza kupoteza matumaini kwa timu hiyo kuweza kutetea taji lake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Salum Ali Haji, alisema katika mchezo wao huo wa juzi waliweza kuimarika katika eneo lililokuwa linawapa tabu la ushambuliaji lakini ulinzi ukawa tatizo lingine.

Alisema walifanikiwa kupata bao la kwanza katika dakika za mwanzoni na la pili katika kipindi cha pili, lakini walishindwa kuimarisha ulinzi katika kulinda mabao yao.

Ali Haji alisema bado ana kazi katika kuhakikisha anaimarisha eneo hilo la ulinzi ambalo litakwenda sambamba na nafasi ya viungo wa kati.

"Bado nahitaji kufanyia kazi jambo la pili kuhakikisha safu ya ulinzi ipo imara, lakini kuhakikisha wachezaji wa kati hawapoteani pale tunaposhambuliwa," alisema.

Hata hivyo, aliwatoa hofu mashabiki wa JKU kuwa timu hiyo itarejea katika mstari uliionyoka kwa kufanya vizuri katika michezo ijayo ya ligi hiyo.

## ZISIKUPITE

### YAMKOMALIA ARNOLD

REAL Real Madrid inavutiwa sana na beki wa Liverpool na England, Trent Alexander-Arnold, 26, wakati huu wanapojiandaa kuimarisha safu yao ya ulinzi. ***(AS)***

### MBEUMO ANYATIWA

KLABU ya Newcastle United imemjumuisha winga wa Cameroon, Bryan Mbeumo, 25, kwenye orodha ya wachezaji inaowataka, huku Brentford ikiweka bei ya pauni milioni 50 kwa mchezaji huyo. ***(Football Insider)***

### KUDUS ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inataka kumnunua winga wa West Ham na Ghana, Mohammed Kudus, 24, kama mbadala wa mshambuliaji wa Ubelgiji, Leandro Trossard (29), ambaye anawaniwa na Klabu ya Al-Ittihad ya Saudia. ***(Mirror)***

### DIAKITE KIPAUMBELE PALACE

MSHAMBULIAJI wa Reims raia wa Ivory Coast, Oumar Diakite, 20, atakuwa kipaumbele cha Crystal Palace ikiwa mazungumzo ya mkataba mpya kati yao na mshambuliaji wao, Mfaransa Jean-Philippe Mateta, 27, yatagonga mwamba. ***(Sun)***

### DORGU AWINDWA UNITED

MANCHESTER United na Chelsea zimeungana na Tottenham Hotspur katika mbio za kumsajili beki wa Denmark, Patrick Dorgu, 20, kutoka Lecce. ***(Football Insider)***

### VINICIUS HAELEWEKI MADRID

REAL Madrid imeanza kutilia shaka dhamira ya Vinicius Jr, 24, katika klabu hiyo na wana wasiwasi kuwa atafikiria kuondoka, huku Al-Hilal wakiwa na nia ya kumsajili mshambuliaji huyo wa Brazil. ***(Sport)***

### NEYMAR ATAKIWA SANTOS

KLABU ya Santos iko kwenye mazungumzo ya kumrejesha Neymar, 32, katika klabu hiyo wakati mkataba wake na Al-Hilal utakapokamilika msimu ujao. ***(AS)***

### BRIEN KUHAMIA LOS ANGELES

KIUNGO wa kati wa England, Lewis O'Brien, 26, anatarajiwa kuhamia Los Angeles FC kwa dau la pauni milioni saba wakati mkopo wake kutoka Nottingham Forest utakapokamilika Januari. ***(Sun)***

### LOPETEGUI HATARINI KUSEPA

KOCHA wa West Ham, Julen Lopetegui anakabiliwa na shinikizo kubwa la kuondoka mapema baada ya kufahamishwa na klabu kwamba matokeo lazima yaboreshwe. ***(Times)***

### KOLO KWA MKOPO

KLABU ya Paris St-Germain na Randal Kolo Muani, 25, wako tayari kwa uhamisho wa mkopo wa Januari, wakiwa na chaguo la kumnunua, na baadhi ya klabu za Ligi England tayari zimewasilisha maombi ya kumsajili mshambuliaji huyo wa Ufaransa. ***(Sky Sport Germany)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH AZUA UTATA MUSTAKABALI WAKE

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah alichapisha ujumbe wa kutatanisha kuhusu mustakabali wake wa Liverpool siku moja baada ya kuifungia timu yake bao la ushindi dhidi ya Brighton.

**Kocha Arne Slot aliendeleza mwanzo wake mzuri wa uongozi kwa ushindi huo wa mabao 2-1, huku mchezaji huyo wa Kimataifa wa Misri akifunga kile ambacho kocha alikiita "Mo Salah Special" kukamilisha ushindi huo.**

Salah mwenye umri wa miaka 32, ni mmoja wa nyota kadhaa ambao klabu ya Merseyside inaweza

### ●●● Asema haijalishi nini kitatokea ila hatasahau kufunga mabao Uwanja wa Anfield kunavyompa...

kuwa katika hatari ya kuwapoteza bila malipo mwishoni mwa msimu huu, huku Trent Alexander-Arnold na Virgil van Dijk pia mikataba yao ikimalizika Juni mwakani.

"Juu ya msimamo ni mahali ambapo klabu hii inafaa," aliandika Salah kupitia mtandao wa kijamii Jumapili.

"Timu zote zinashinda mechi, lakini bingwa ni mmoja tu, ndio tunataka, asante kwa sapoti yenu.

"Haijalishi nini kitatokea, sitasahau kufunga kwenye Uwanja wa Anfield kunavyonipa hisia kali."

Salah aliiambia Sky Sports mwanzoni mwa msimu huu kwamba huu unaweza kuwa msimu wake wa mwisho akiwa na Liverpool, timu ambayo alijiunga nayo mwaka 2017 akitokea AS Roma.

Baada ya ushindi wake katika Uwanja wa Anfield Jumamosi, sasa ana mabao 164 katika mechi 273 alizoichezea klabu hiyo.

Alishinda Ligi Kuu England chini ya Jurgen Klopp mwaka 2020 na Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019, na vile vile Kombe la FA na lile la Carabao.

HABARI MICHEZO

# OLMO ATAKA ZAIDI BARCA




**BARCELONA,** Hispania

DANI Olmo amesema anataka "zaidi" baada ya kucheka na nyavu mara mbili katika mchezo wake wa kwanza tangu Septemba wakati Barcelona ilipoilaza Espanyol mabao 3-1 kwenye mchezo wa Jumapili Dabi ya Kalalunya iliyopigwa Uwanja wa Olympic.

Raphinha pia alifunga huku Barca wakisonga mbele kwa pointi tisa kileleni mwa Ligi Kuu Hispania baada ya mechi 11. Espanyol walipata bao la kufutia machozi kupitia kwa Javi Puado.

"Ninajisikia vizuri," alisema Olmo, ambaye hivi karibuni alirejea kutoka kwenye jeraha la muda wa mwezi mzima, akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilitarajia sana kurudi na kuweza kuisaidia timu uwanjani. Nimerudi, nikifurahia, kucheza, kushinda ... na nataka zaidi."

Olmo, aliyesajiliwa kwa euro milioni 60 majira ya joto kutoka RB Leipzig, sasa ana mabao matano katika mechi tano za ligi.

Kurejea kwa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Hispania kunaongeza mwelekeo mwingine kwenye safu ya ushambuliaji.

Kwa jumla, Barca sasa wamefunga mabao 40 kwenye ligi msimu huu na ndiyo timu pekee katika ligi tano bora za Ulaya kuwa na wachezaji wanne kwa angalau mabao matano: Robert Lewandowski (14), Raphinha (7), Lamine Yamal (5) na Olmo (5).

"Sisi ni timu yenye malengo mengi ndani yake," aliongeza Olmo.

"Washambuliaji wa mbele na wa kati wanaosonga mbele wanaweza kuchangia katika suala hilo. Tunaweza kucheza moja kwa moja na tunatengeneza nafasi nyingi."

Mabao yote mawili ya Olmo yalifika kipindi cha kwanza, la kwanza kupitia pasi nzuri ya Yamal na la pili kutoka pembeni mwa eneo la hatari, huku Kocha wa Barca, Hansi Flick, akisifu uwezo wake wa kufunga mabao.

"Anajua jinsi ya kufunga mabao, hii ilikuwa muhimu sana kwetu leo," alisema Flick katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo.

# Fernandes amwomba msamaha Ten Hag

**MANCHESTER,** England

BRUNO Fernandes amefichua kuwa alimpigia simu Erik ten Hag kuomba msamaha baada ya Mholanzi huyo kutimuliwa na Manchester United.

Fernandes alifunga mkwaju wa penalti wakati United walitoka sare ya bao 1-1 na Chelsea katika mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu England tangu Ten Hag atimuliwe Jumatatu iliyopita.

"Wakati wowote unapoona kocha akienda lazima uchukue lawama kwako mwenyewe, ni kwa sababu timu haifanyi vizuri," alisema Fernandes akiambia Sky.

"Ni rahisi kumwondoa kocha kuliko wachezaji 15. Nilizungumza na kocha (Ten Hag) na kumuomba msamaha, nilikata tamaa kwamba ameenda na nilijaribu kumsaidia. Sikuwa nafunga mabao.

"Si vizuri kwa mtu yeyote kwenye klabu wakati kocha anapoondoka. Timu si bora, matokeo si bora na yeye ndiye anayelipa."

Baada ya kuondoka kwa Ten Hag, United wameifunga Leicester kwenye Kombe la Carabao na kutoka sare na Chelsea kwenye Ligi Kuu ya England chini ya kocha wa muda, Ruud van Nistelrooy.

Van Nistelrooy ana michezo mingine miwili ya kuinoa kabla ya Ruben Amorim kuchukua hatamu Novemba 11.

Hata hivyo, Van Nistelrooy alikiri imekuwa wiki "ngumu" katika klabu hiyo na kusema wamelazimika "kujitazama kwenye kioo" baada ya kuanza vibaya msimu huu.

"Imekuwa ngumu sana kutoka kwa kumbukumbu hadi leo, siku sita, hali ya hisia," alisema Van Nistelrooy. "Inasikitika sana kuona Erik akiondoka.

"Inabidi uanze kuzingatia kuwaweka vijana tayari kwa Leicester kwa sababu watu 75,000 wanajitokeza hapa Old Trafford na wanahisi wana wajibu wa kufanya zaidi vizuri.

"Wanaangalia kwenye kioo na majibu yao wakati huo na leo ya kufikiria juu ya mambo."

Mustakabali wa muda mrefu wa Van Nistelrooy bado haujulikani baada ya Amorim kueleza nia yake ya kuleta wakufunzi wake Old Trafford.

# Maresca ashangaa Martinez kutopewa kadi nyekundu

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Chelsea, Enzo Maresca, amesema Lisandro Martinez wa Manchester United alipaswa kutolewa nje kwa kadi nyekundu kwa faulo aliyomfanyia Cole Palmer ambapo beki huyo alipewa ya njano wakati wa sare ya bao 1-1 kwenye mchezo wa Ligi Kuu England katika Uwanja wa Old Trafford Jumapili.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Argentina, Martinez alipewa kadi hiyo na mwamuzi Robert Jones dakika tatu kabla ya kumalizika mechi hiyo kwa kumchezea rafu Palmer kwa kumrukia kwenye goti fowadi huyo wa England.


Mwamuzi Msaidizi wa VAR, Michael Salisbury, alikagua changamoto hiyo kabla ya kutangaza kwamba uamuzi wa mwamuzi Jones, uwanjani ulikuwa sahihi kwa sababu, kwa mujibu wa kanuni za Ligi Kuu England, ilionekana kuwa "changamoto ya kutojali na si mchezo mbaya."

Nahodha wa zamani wa United, Roy Keane, akiwa mchambuzi wa mchezo huo kupitia Sky Sports, alisema, "Martinez ni kijana mwenye bahati. Ni mchezo mbaya," na Kocha wa Chelsea Maresca alidai kwamba alimwambia mwamuzi kwamba Martinez alipaswa kutolewa nje kwa kadi nyekundu.

"Walinionesha changamoto kabla ya mkutano na waandishi wa habari," alisema Maresca akiwaambia waandishi wa habari.

"Nadhani ni wazi kwa sisi sote na wao viongozi walichukua uamuzi tofauti.

"Wakati hakuna nia ya kutafuta mpira na unaenda tu kwa mchezaji, ni nyekundu. Yeye mwamuzi hakusema chochote, lakini unapoenda kwa mchezaji au miguu, hakuna shaka juu ya uamuzi huo. Nadhani ni wazi kabisa ilipaswa kuwa nyekundu."



# HABARI MICHEZO

## Kagoma matibabu wiki tatu zaidi

**Na Faustine Feliciane**

KIUNGO wa Simba, Yusuph Kagoma, ataendelea kuwa nje ya uwanja kwa angalau wiki tatu zaidi akiendelea kupata matibabu ya jeraha lake la mguu.

Kagoma hajaonekana uwanjani tangu baada ya mchezo wa dabi ya kariakoo dhidi ya Yanga uliochezwa Oktoba 19, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao hakumaliza baada ya kuumia na kutolewa nje.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ali, alisema nyota huyo bado yupo kwenye matibabu ya wiki tatu zaidi.

"Nyota wetu Yusuph Kagoma bado yupo kwenye matibabu, ana wiki tatu zaidi za matibabu na inshallah atarejea uwanjani kuendelea na majukumu yake," alisema Ahmed.

Alisema baada ya kupata majeraha alianza matibabu na taarifa alizonazo ni kuwa ana wiki tatu za matibabu kabla ya kuanza kurejea uwanjani.

"Wanasimba wasiwe hofu, mchezaji wetu anaendelea na matibabu, najua wengi wanatamani kumuona uwanjani, niwahakikishie atarejea hivi karibuni," aliongeza kusema Ahmed.

Kagoma tangu kutua Simba kwenye dirisha lililopita akitokea Singida Big Stars, ameonesha kiwango bora na kuwa kipenzi cha mashabiki wa klabu hiyo.

## Gamondi ataja

INATOKA UK. 24

cheza mechi mbili mfululizo kwa siku mbili, lakini nakumbuka msimu uliopita zilichezwa mechi mbili hapo hapo, tulicheza sisi mechi moja ya kimataifa leo na kesho yake Simba wakacheza pia, sina maana Uwanja wa Azam Complex ni mbaya hapana, ila kucheza mchezo wa nyumbani kwenye uwanja wa mpinzani wako ni kumpa faida," alisema Gamondi.

Alisema kwa sasa yamepita na anachoangalia ni kukiandaa kikosi chake kwenye mchezo unaofuata dhidi ya Tabora United utakaopigwa kesho kutwa, Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, ukiwa ni wa kumi kwa timu hiyo.

Pamoja na kufungwa, Yanga bado inaongoza ligi ikiwa na pointi 24, ikifuatiwa na Singida Black Stars yenye pointi 23, Simba nafasi ya tatu na pointi zake 22, Azam FC ikisimama nafasi ya nne baada ya kukusanya pointi 21, huku Fountain Gate ikwa kwenye nafasi ya tano na pointi zake 17.

# KAMATI KUAMUA UTATA PENALTI ILIYOVUNJA MECHI LIGI KUU Z'BAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya mchezo wa Ligi Kuu Zanzibar kati ya Mwenge SC na Uhamiaji FC kushindwa kuendelea na kuvunjika kabla ya dakika nne za nyongeza ili kukamilisha dakika 90 za mpira kuchezwa uwanjani katika Dimba la Finya, Kisiwani Pemba juzi, maamuzi sasa yatatolewa ndani ya saa 72, imeelezwa.

Mchezo huo ambao ulichezwa mwishoni mwa wiki ulivunjika wakati timu hizo zikiwa bado hazijafungana, kutokana na Uhamiaji FC kugomea mchezo huo baada ya wapinzani wao kupewa penalti.

**Uhamiaji FC ilitoka uwanjani baada ya mwamuzi wa mchezo huo kutoa penalti kwa timu ya Mwenge SC tukio lililolalamikiwa na benchi la ufundi lao na kuamua kutoka nje ya uwanja, hivyo mechi kuvunjika.**

Akithibitisha juu ya tukio hilo lililotokea Finya Kisiwani Pemba, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Shirikikisho la Soka Zanzibar, Issa Kassim, alisema bodi kupitia Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi, itapitia ripoti ya mwamuzi juu ya mchezo huo na kutoa maamuzi.

Alisema kamati hiyo itakutana ndani ya saa 72 ili kuhakikisha inatoa maamuzi hayo kwa haraka kabla ya kuanza mzunguko wa 10 wa ligi hiyo.

"Maamuzi yatotoka haraka ndani ya muda wa saa 72 kama inavyosema kanuni, na kitendo kilichofanyika kwa ngazi hii ya Ligi Kuu si kizuri na hakina afya," alisema.

Aidha, alisema Bodi ya Ligi imewataka viongozi wa klabu kupitia mabenchi yao ya ufundi kuzingatia nidhamu mchezoni pamoja na kuzisoma kanuni.

Alisema kupitia matukio ambayo yanajitokeza katika Ligi Kuu Zanzibar hasa ya kinidhamu, mengi yao yanasababishwa na mabenchi ya ufundi.

Kassimu alisema Bodi ya Ligi kwa kushirikiana na kamati ya ufundi inatarajia kufanya kikao maalum na walimu wa timu zote za Ligi Kuu katika kipindi hiki ambacho ligi hiyo inaendelea ili kuhakikisha matukio kama hayo hayajirudii tena.

**TUTA HILO...**



Mshambuliaji wa Manchester United, Rasmus Hojlund, akichezewa faulo na kipa wa Chelsea, Robert Sanchez, ambayo ilizaa penalti iliyozamishwa nyavuni na Kiungo Bruno Fernandes, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# *Fadlu: Dabi ijayo Simba, Yanga itaamua*

INATOKA UK. 24

Kuhusu mchezo dhidi ya KMC FC, utakaochezwa kesho Uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam, Fadlu alisema haitokuwa rahisi, lakini pointi tatu muhimu sana kujiweka katika mazingira mazuri.

"Tuna waheshimu wapinzani wetu, tunahitaji kufanya vizuri katika mchezo wetu dhidi ya KMC mara ya mwisho tulitoka nao sare ya mabao 2-2, hatutaki kujirudia," alisema.

Hata hivyo, Fadlu hakuwapo kwenye mchezo huo badala yake aliyekiongoza kikosi hicho wakati huo alikuwa ni Mbrazil, Roberto Oliveira Robertinho.

Fadlu aliongeza: "KMC ni timu nzuri na wapo kwenye kiwango kizuri, watakuwa kwenye uwanja wao hivyo natarajia ushindani mkubwa kutoka kwao, kama timu tumejiandaa vizuri na tunaendelea na maandalizi yetu".

Alisema kuwa baada ya safari ndefu kutoka Kigoma, walifanya mazoezi mepesi na sasa wanaendelea na maandalizi ya mchezo huo.

"Tulifanya kazi kubwa sana Kigoma, wachezaji wangu walijituma sana na tulifanikiwa kupata ushindi dhidi ya Mashujaa, baada ya hapo niliwataka wachezaji wasahau matokeo hayo na kuweka mipango yetu kwenye mchezo na KMC," alisema Fadlu.

Alisema kwenye mchezo wa kesho wataingia uwanjani wakiwa na lengo la kuondoka na pointi zote tatu, lakini hawatawadharau wapinzani wao hao.

"Nimewaangalia KMC kwenye baadhi ya michezo yao, ni timu nzuri, ni lazima wachezaji wangu wajitoe na kupambana kama walivyofanya Kigoma ili tufikie lengo letu la kuondoka na pointi zote tatu," alisema Fadlu.

Rekodi zinaonesha timu hizo zimekutana mara 12 tangu KMC ilipopanda daraja, huku takwimu zikibainisha kuwa Simba imeshinda mara 10 na sare mbili, huku timu hiyo inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni ikiwa haijawahi kupata ushindi wowote dhidi ya Wekundu wa Msimbazi hao.

Iwapo Simba itashinda mchezo wa kesho itafikisha pointi 25 na kukwea hadi kileleni mwa msimamo huku ikisubiri mchezo wa Alhamisi ijayo, ambao watani zao wa jadi, Yanga wenye pointi 22, watakapocheza dhidi ya Tabora United, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Michezo

Jumanne Novemba 5, 2024

Nipashe



Salah azua utata mustakabali wake UKURASA 21



Gamondi

# Gamondi ataja timu za ubingwa Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Asema ni nne ambazo kila moja inaweza kuchukua pointi kwa mwenzake, huku...

PAMOJA na kufungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC, Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameeleza kufurahishwa kuongezeka kwa ushindani kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam, Gamondi, alisema kwa sasa kuna timu nne ambazo zina wachezaji bora, wenye uzoefu ambazo zinaweza kushinda mchezo wowote na kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara.**

Amezitaja timu hizo kuwa ni Simba, Yanga, Azam FC na Singida Black Stars, ambazo zimefanya usajili bora na kufanya vikosi vyao kuwa tishio.

"Msimu huu timu zimejipanga, zimekuwa bora, lakini kuna timu nne ambazo zina uzani wa juu na yoyote inaweza kuifunga timu yoyote na kuchukua ubingwa. Tumeona Azam imeshinda, ina wachezaji wazuri, Simba hali kadhalika ni timu bora msimu huu, halafu msimu huu imekuja timu nyingine ngumu nayo ni Singida Black Stars.

Timu hizi nne zimefanya kuongezeka kwa ugumu wa ligi na ubora, hivyo inabidi yeyote anayeutaka ubingwa kufanya kazi ya ziada," alisema Gamondi.

Hata hivyo, Gamondi alilalamikia mchezo wao dhidi ya Azam FC ambao kwa Yanga ulikuwa wa nyumbani kwenda kucheza kwenye uwanja wa wapinzani wao.

Alisema hakuona sababu mchezo huo kutochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kwa sababu wao ndiyo walikuwa wenyeji.

"Mimi sijafurahi kwa hiyo, niwe muwazi, kucheza mechi yetu ya nyumbani kwenye uwanja wa wapinzani wetu.

"Wanasema Uwanja wa Benjamin Mkapa haiwezekani ku

INAENDELEA UKURASA 23

# Fadlu: Dabi ijayo Simba, Yanga itaamua bingwa

**Adam Fungamwango na Faustine Feliciane**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema anaamini kuwa dabi ya mzunguko wa pili kati ya timu yake dhidi ya Yanga ndiyo inaweza kumpata bingwa wa Tanzania Bara, hivyo hana presha na ubingwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, kocha huyo alisema kwa sasa anachoangalia ni kuhakikisha timu yake inapata pointi tatu kwenye kila mchezo ili kufikia malengo.

Alisema anafurahishwa sana na viwango vya wachezaji wake kwa jinsi wanavyojitoa na kupambana, ingawa changamoto kubwa anaiona kwa waamuzi ambao hawawalindi kwa kuruhusu wapinzani kuwachezea vibaya hata ndani ya eneo la hatari, lakini wamekuwa wakifumba macho.

"Nafurahishwa na viwango vya wachezaji wangu, wamekuwa wakipambana, lakini nimeongea nao na kuwaeleza juu ya kucheza bila ya kukata tamaa ndani ya uwanja kwa kuwa mpira hauishi hadi filimbi ya mwamuzi inapopigwa, licha ya kwamba wanakutana na changamoto ya waamuzi ambao wamekuwa hawawalindi, wamekuwa wakichezewa vibaya na wapinzani nje na ndani ya boksi, lakini wanaangalia tu.

"Kuhusu ligi bado mbio ndefu ni mapema sana kukata tamaa kuhusu ubingwa, nadhani mzunguko wa pili tutakapomaliza dabi kila kitu kitakuwa wazi na kupata mwanga wa mbio za ubingwa," alisema Fadlu.

Alisema kwa sasa atakuwa anafanya mabadiliko ya mfumo kulingana na mpinzani watakayekutana naye, kwani amegundua kila timu inakuja na malengo na mfumo tofauti jinsi ya kuwakabili.

"Wengine hawaji kutafuta ushindi, wanakuja kutuzuia sisi kupata ushindi," alisema.

INAENDELEA UKURASA 23



Fadlu

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >